# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 2 | Septemba 11, 2022 JARIDA LA JUMAPILI BILA MALIPO





# KILICHOPONZA UHURU

**Nyamakima - eneo maarufu zaidi kwa biashara haramu Kenya, lenye kila aina ya bidhaa - kutoka zilizo ghushi hadi za magendo zinazoshukiwa kutolipiwa ushuru. Biashara hii inayopendwa na wengi inaaminika ndiyo iliyommaliza kisiasa Rais Kenyatta.**

# EVOLVE

KENYA TOP 100 MID-SIZED COMPANIES Business Daily KPMG

## BECAUSE YOUR BUSINESS DOESN'T STAND STILL – IT EVOLVES

Each stage of your business cycle presents its own set of opportunities and challenges. Do you have what it takes to be successful at each stage? Enter the 2022 Top100 Midsized Companies Survey and take your seat among the great.

**Benefits:**

- Recognition for companies that have successfully redefined their business and remained agile in an increasingly uncertain business landscape.
- Access to an industry benchmarking report and thought leadership to all participating companies.
- Opportunities to network with peers and sponsors through the exclusive Top100 Mid-Sized Companies conference and gala dinner.
- Winners will be eligible to use the 2022 Kenya Top100 Mid-Sized Companies Club logo.

Survey closes on 9 September 2022


**Submit your entry at: www.eastafricatop100.com**

**Kenya100@kpmg.co.ke**

**020 280 6000**







**Be seated among the great.**

Business Daily KPMG

In partnership with:

IFC International Finance Corporation WORLD BANK GROUP Creating Markets, Creating Opportunities

#Top100KE Top100SME @Top100SME

kauli ya mhariri

# Sura mpya ya Kenya: Ahadi na hatari ya enzi mpya



Mutuma Mathiu

Kwa binadamu, ushirikiano ni hitaji kwa mageuzi. Katika kitabu chake cha kuvutia na maarufu ambacho kimenukuliwa kwa upana Sapiens: A Brief History of Humankind, msomi kutoka Israeli Yuval Noah Harari anasema kufuatia kuibuka kwake - zao la mabadiliko ya maumbile, babu yetu, Homo erectus, hakubadilika kwa karibu miaka milioni mbili. Hata vifaa vya mawe alivyotengeneza na lengo la kuvitengeneza - kuvunja mifupa kupata uboho ndani yake - havikubadilika kwa miaka hiyo milioni mbili!

Kisha kati ya miaka 70,000 na 30,000 iliyopita, cheche ziliwaka katika ubongo wa mababu zetu na wakaanza kufikiria, kufikiria kwa makini, na kuwasiliana miongoni mwao.

Mageuzi ya lugha wakati wa iliyoitwa Mageuzi ya Utambuzi ya enzi hizo, yaliturhusu kuwasilisha, sio tu ujumbe kama vile kuonyana kuhusu hatari, ambako kila mnyama anaweza kufanya, lakini habari kuhusu kila mmoja na kuturahishia kutangamana katika njia thabiti zaidi.

Lugha pia ilituruhusu kuunda dhana ambazo hazikuwa na ukweli, mambo ambayo yalidumu tu katika akili zetu – Harari anatoa mfano wa kampuni na nchi - akiashiria makundi makubwa, mamilioni ya binadamu wanaweza kushirikiana. Wachina bilioni moja wanaweza kuwa waaminifu na kushirikiana kwa ajili ya China, katika fikira zao.

Kwa kushirikiana katika makundi makubwa, binadamu ameweza kutawala viumbe wengine na kupinda asili kukidhi mahitaji yake. Mabadiliko katika tabia siku hizi hayahitaji mageuzi ya maumbile; inaweza kuwa tabia zetu zinazohitaji mageuzi yetu ya maumbile.

> **Changamoto ya Ruto ni kuunganisha nchi nyuma yake. Wito mkubwa wa serikali yake sio kulipiza kisasi, kisasi duni na "kujihisi mshindi" kama mchanganuzi mmoja alivyouita, mbali ni unyenyekevu na shukrani kwa kazi ngumu iliyo mbele yake.**

Kikomo cha nguvu za mwanadamu kinatoka kwa kukosa kwake kushirikiana katika kiwango cha viumbe; iwapo wote wangeungana, wanaweza kushinda kifo, ulimwenguni, na pengine muda wenyewe.

Kuna mafunzo kutoka kwa mababu zetu ambayo serikali mpya ya Rais-mteule William Ruto inafaa kusoma. Inarithi changamoto nyingi za ndani na za nje.

Hali ya dunia ya zamani, inayotawaliwa na mataifa ya Magharibi, ukuaji wa maendeleo, amani na utulivu zinabadilishwa katika kichwa chake. Majanga ya ulimwengu na Ulaya zimesababisha hali ngumu ya uchumi. Mataifa mapya yenye nguvu yanapita yale yaliyostawi: India imepita Uingereza kuwa nchi ya tano yenye uchumi mkubwa ulimwenguni. Nchi mpya kwa nguvu za kijeshi kama China zinakaribia kupinga falme za kisasa za Magharibi kudhibiti ulimwengu.


Matukio haya ya ulimwengu yanaathiri hali ya Kenya wakati huu na siku zijazo. Ndani ya nchi, matarajio ni makubwa. Mamilioni ya watu hawana kazi na vijana masikini wanatarajia maisha yao yabadilike - usiku mmoja. Watumishi wa umma kama vile polisi na walimu wanatarajia watimiziwe ahadi ya kuongezwa mshahara waliyopewa wakati wa kampeni.

Mlipa hushuru aliyeumia kwa muda mrefu anasubiri afueni. Wamiliki wa biashara ndogo na wasio na ajira wanasimama mlangoni wakisubiri Hazina ya Mahsla. Wale wanaoitwa hoehae wanatazama barabara, wakitarajia kusafirishwa kutoka chini hadi juu.

Ahadi hizi zinaweza, na bila shaka, kutimizwa kikamilifu. Lakini itachukua zaidi ya watu milioni saba waliopigia kura Kenya Kwanza. Changamoto ya Ruto ni kuunganisha nchi nyuma yake. Wito mkubwa wa serikali yake sio kulipiza kisasi, kisasi duni na "kujihisi mshindi" kama mchanganuzi mmoja alivyouita, mbali ni unyenyekevu na shukrani kwa kazi ngumu iliyo mbele yake. Zawadi ya ushindi uliopingwa ni kuu. Ni ushirikiano, sio ugomvi, uliotufikisha tulipo kama taifa na kama watu.

*mmutuma@ke.nationmedia.com*

## Yaliyomo

5 HESABU, SI UTARATIBU

Uamuzi wa Mahakama ya Upeo katika kesi za chaguzi za urais za 2013 na 2017 zilisababisha tetesi za kisiasa kuhusu jinsi majaji walifikia maamuzi yao.

8 RUTO TAYARI KWA KAZI

Iwapo Ruto atatimiza ahadi yake ya kuunda tume ya kuchunguza waliotumia serikali vibaya, atakuwa amelenga himaya ya biashara za familia ya Kenyatta.

10 RAILA: AMETOKA?

Anapofikiria hatua mpya baada ya kushindwa, minong'ono kuhusu mrithi wa Raila Odinga imeanza katika ngome yake.

22 NDOTO YA GIDEON YAZAMA

Matumaini ya mwenyekiti wa Kanu ya kurithi ufalme wa kisiasa wa baba yake katika Bonde la Ufa yadidimia baada ya kushindwa vibaya katika uchaguzi wa hivi majuzi.



Darubini Ya Wiki

Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno

**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Mutuma Mathiu** Mhariri Mkuu
**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji
**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Benjamin Situma, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

# kurunzi ya Kenya

■ Rais - mteule Ruto tayari kushika hatamu



Rias Uhuru Kenyatta (kushoto) akizungumza na Naibu Rais William Ruto katika Chuo cha Kitaifa cha Mafunzo ya Kijeshi, eneo la Karen, mnamo Mei 3, 2017. EVANS HABIL I NATION

## Kutoka Kenyatta hadi 'Rais wa Tano'

Maandilizi ya kumuapisha William Ruto kuwa Rais wa tano wa Jamhuri ya Kenya yanaendelea.

Taarifa kutoka kwa Kamati ya Mpito ya Ofisi ya Rais inaonyesha kuwa sherehe hiyo itafanywa Jumanne katika uwanja wa Kimataifa wa Michezo wa Moi, Kasarani, kati ya saa nne mchana na saa nane adhuhuri.

Karibu viongozi wa nchi 40, akiwemo Rais Yoweri Museveni wa Uganda, Evariste Ndayishimiye wa Burundi, Paul Kagame wa Rwanda na Salva Kiir wa Sudan Kusini watahudhuria hafla hiyo. Ibara 141 ya Katiba inasema Rais-mteule ataapishwa hadharani mbele ya Jaji Mkuu, Jumanne ya kwanza kufuatia siku 14 baada ya kutangazwa kwa matokeo ya kura ya urais iwapo hakuna kesi ya kuyapinga itawasilishwa.

Na iwapo kesi itawasilishwa, siku ya saba kufuatia tarehe ambayo Mahakama ya Upeo itatoa uamuzi wake kutangaza uchaguzi kuwa halali.

Baada ya Dkt Ruto kula kiapo, Rais Kenyatta atamkabidhi upanga, kuashiria mabadiliko ya mamlaka kama Amiri Jeshi Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi Kenya.

■ Kwa kulinda demokrasia Amerika

## Obama na mkewe wapata michoro yao

Aliyekuwa Rais wa Amerika, Barack Obama na Mama wa Taifa, Michelle Obama, hatimaye wamepata michoro yao ya Ikulu ya White House, baada ya miaka minne ya kupuuzwa na Donald Trump, katika hafla iliyojaa hisia na ambayo pia ilitajwa kuwa ya kulinda demokrasia Amerika.

Michoro hiyo, ilifunguliwa na Obama na mkewe wenyewe.

Vifijo na nderemo zilisikika katika ukumbi wa East Room walipokuwa wakiondoa vitambaa vya samawati vilivyofunika kazi hiyo ya sanaa.

Obama, rais wa kwanza wa nchi hiyo mwenye asili ya Kiafrika, alichorwa na Robert McCurdy, akionekana wima, akiwa ameweka mikono yake mifukoni, suti yake nyeusi ikichomoka vyema na kivuli kikiwa katika nusu ya uso wake. Michelle, aliyechorwa na Sharon Sprung, alipozi kwa rinda rangi ya bluu nyepesi, akiketi kwenye sofa ya rangi nyekundu. Obama alitania kwamba umakinifu wa McCurdy ulimaanisha "alikataa kuficha nywele zake nyeupe", lakini akasema staili aliyotumia iliondoa mtindo ambao marais "mara nyingi hupakwa rangi" na "kujipata katika hadhi ya kizushi, hasa baada ya kuondoka na watu kusahau mambo yao ambayo hawakutaka".

Shangwe ziliendelea wakati wa hotuba ya Rais Joe Biden iliyoanzisha hafla hiyo na zikaongezeka baada ya Obama kuingia jukwaani.



Aliyekuwa Rais wa Amerika Barack Obama ampiga busu aliyekuwa Mama Taifa Michelle Obama wakati wa sherehe ya kufungua michoro yao rasmi ya Ikulu ya White House, eneo la East Room, Ikulu ya White House, jijini Washington, DC, Septemba 7.

■ EACC yawapa maafisa siku 30 kutimiza sheria

## Viongozi wapya kutangaza utajiri wao




Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi imeagiza maafisa wapya wa serikali kutangaza utajiri wao ndani ya siku 30. Matangazo hayo yanafaa kujumuisha mali ya wachumba na watoto wao. EACC ilitaja sheria vya Maadili ya Maafisa wa Umma, kuhusu hitaji la lazima la maafisa hao kutangaza mali yao siku 30 baada ya kuingia ofisini, na kukosa kufanya hivyo au kudanganya katika tangazo hilo, ni kosa la uhalifu na wanaweza kutozwa faini isiyozidi Sh1 milioni, au kufungwa jela hadi mwaka mmoja au adhabu zote mbili wakipatikana na hatia.

Kenya ni miongoni mwa nchi za kwanza ulimwenguni kuidhinisha Azimio la Umoja wa Mataifa Dhidi ya Ufisadi, ambalo lilipelekea kuanzishwa kwa Sheria ya Maadili ya Maafisa wa Umma (POEA).

■ McIlroy akiri kuachana na wenzake

## Kuhamia LIV Golf kwazua utengano



Rory McIlroy amekiri uhusiano wake na wenzake kadhaa wa Ryder Cup umeharibika sana kwa sababu yao kuhamia LIV Golf. Wanachama watano wa timu hiyo ya Ulaya iliyoshindwa katika dimba la Whistling Straits mwaka jana, wamejiunga na timu iliyojitenga ambayo inafadhiliwa na Saudi Arabia, pamoja na Henrik Stenson, ambaye uamuzi wake ulimfanya akose unahodha katika shindano la mwaka ujao Roma. Wanne kati ya watano hao —Ian Poulter, Lee Westwood, Sergio Garcia na Bernd Wiesberger — walikuwa miongoni mwa wanachama wa LIV katika mashindano ya PGA, Ulaya.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Kenya

USHAHIDI

# HESABU HAINA KONA – MAJAJI

*Mahakama ya Upeo ilidumisha ushindi wa Ruto dhidi ya Raila katika uchaguzi wa urais. Walalamishi walishindwa jinsi hesabu ya kura katika fomu kutoka vituo vya kupigia kura ilitofautiana na matokeo yaliyotangaza na Chebukati*

• Na MACHARIA GAITHO

Uamuzi wa Mahakama ya Upeo katika kesi za kupinga matokeo ya chaguzi za urais 2013 na 2017 uliibua tetesi nyingi za kisiasa kuhusu jinsi majaji walifikia maamuzi yao na kuzua shaka kuhusu Uhuru wa Idara ya Mahakama.

Uamuzi wa 2022 mnamo Jumatatu, uliodumisha ushindi wa William Ruto dhidi ya Raila si tofauti. Tayari umegeuka mada ya mjadala mkali, wengi wakikerwa na lugha kali iliyotumiwa na Jaji Mkuu Martha Koome dhidi ya walalamishi katika kesi hiyo, na maswali kuhusu iwapo uamuzi huo ulizingatia ushahidi ama kilikuwa kile wengi wanataja kuwa uamuzi wa kisiasa.

Hata kabla ya uamuzi kamili kutolewa ili kuchunguzwa kwa kina kubaini sababu zilizopelekea uamuzi huo wa pamoja, Koome aliibua shaka kwa kuuzungumzia hadharani.

Jaji Mkuu alikuwa akihutubia watu kwenye mazishi katika Kaunti ya Meru Jumatano alipotumia fursa hiyo kutetea Mahakama ya Upeo, akisema uamuzi huo "ulitolewa kwa ajili ya kulinda uhuru wa taasisi huru, hasa Idara ya Mahakama. Haukutokana na uwezo au nguvu zetu kama korti, bali kwa sababu ya Mungu mwaminifu tunayemtumikia."

Huenda kuna watu watajiuliza ni kwa nini alitaja Mungu katika jamii ambapo maamuzi ya korti yanatarajiwa kuzingatia sheria badala ya ufuasi wa kidini, kisiasa au makundi mengine. Kauli ya Koome ya kulinda uhuru wa Idara ya Mahakama haikuelezewa, lakini inaonyesha kuwa mbali na tetesi zilizowasilishwa kortini na walalamishi na washtakiwa, huenda majaji walitaka kusisitiza uhuru wao dhidi ya majaribio ya kuwaingilia au kuwatisha.

Ni katika muktadha huo ambapo baada kutangaza uamuzi huo, Naibu Jaji Mkuu Philomena Mwilu, aligusia kuhusu watu fulani waliojaribu kuwapigia simu walipokuwa wakitayarisha uamuzi wao lakini wakapuuza.

Katika muktadha huo huo, mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka, Wafula Chebukati, ilifichua habari za kushangaza wakati wa kesi hiyo, kuwa wanachama wa Kamati ya Kitaifa ya Ushauri kuhusu Usalama ilijaribu kumshawishi 'afinyange' matokeo ya uchaguzi ili kumpa ushindi Raila badala ya Ruto.

Katika hati kiapo, Bw Chebukati alidai kuwa Katibu Mkuu katika Afisi ya Rais, Kennedy Kihara, Naibu Mkuu wa Majeshi, Francis Ogolla, Inspekta Jenerali wa Polisi, Hilary Mutyambai na Wakili Mkuu wa Serikali, Kennedy Ogeto walifika ofisini mwake katika kituo cha kitaifa cha kujumuisha kura Bomas of Kenya wakimtaka abadili matokeo kwa misingi ya usalama wa kitaifa. Alidai pia wafanyakazi wa IEBC walihangaishwa, kutishwa na kukamatwa kiholela, na bila kutoa ushahidi wowote, akajaribu kuhusisha mauaji ya afisa wa tume hiyo na uchaguzi. Hata hivyo, bila kutoa ushahidi, Bw Chebukati alijaribu kuhusisha mauaji ya afisa mmoja wa kusimamia uchaguzi na uchaguzi.

**Iwapo ni kweli majaji pia walisukumwa, tunasubiri kuona yatakayojiri katika malalamishi na ripoti rasmi mbali na matamshi yaliyotolewa ambayo hayakuwa na ushahidi.**

Madai ya Chebukati, ingawa hayakuthibitishwa, yalitumiwa na washirika wa Ruto kuthibitisha madai ya majaribio ya wenye ushawishi serikalini, uzima safari yake ya Ikulu.

Iwapo kweli majaji wa Mahakama ya Upeo walishinikizwa, tunasubiri kuona yatakayojiri katika malalamishi na ripoti rasmi mbali na matamshi yasio na ushahidi.

Lakini kwa sasa Jaji Mkuu Koome na wenzake sita, Mwilu, Mohamed Ibrahim, Smokin Wanjala, Njoki Ndung'u, Isaac Lenaola na William Ouko wanafaa kujiandaa dhidi ya ukosoaji mkubwa kabla ya kutoa uamuzi kamili. Dalili za yanayojiri zilioneka pale Rais Uhuru Kenyatta alipokubali uamuzi huo shingo upande.

Zaidi ya majibu ya Raila na mgombea-mwenza Martha Karua kwamba "sikubaliani na uamuzi lakini nimeupokea", Uhuru alilaumu Mahakama ya Upeo kwa kuamua kwa njia moja 2017 na njia tofauti wakati huu, akiwataka Wakenya wahakikisha taasisi zinafanya maamuzi yanayoeleweka na kuaminika.

"Je, suala kuu ni idadi au utaratibu uliofuatwa?" akauliza katika hotuba yake ya kwanza tangu kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi. "Taasisi inaweza kuamua kwa njia moja katika uchaguzi na kwa njia nyingine katika uchaguzi mwingine bila kuibua maswali," akauliza.

Alikuwa akirejelea tukio la kihistoria mnamo 2017 ambapo ushindi wake katika uchaguzi wa urais ulibatilishwa na Mahakama ya Upeo chini ya Jaji Mkuu David Maraga, kwa misingi ya utaratibu uliojaa dosari.

Kwenye kesi ya majuzi, Koome na wenzake hawakuzingatia sana utaratibu ama ushahidi, na badala yake waliegemea hesabu ya kura. Hiyo ndiyo sababu kesi ya Raila ilitupwa kwa kushindwa kutoa ushahidi wa hesabu ya kura katika fomu kutoka vituo vya kupigia kura iliyotofautiana na matokeo yaliyotangazwa na Chebukati.



PICHA | DENNIS ONSONGO

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

■ WAFANYABIASHARA WALIVYOZIMA MPANGO WA UHURU

# MAMILIONEA WA NYAMAKIMA

*Eneo hili la biashara lenye shughuli nyinngi, katikati ya barabara za River Road na Kirinyaga, Nairobilimekuwa likivuma kinachojulikana kama moyo wa kibiashara wa Mlima Kenya.*




**Magari ya Usafiri wa Umma katika eneo la Nyamakima, Nairobi, Septemba 7. Tlilitekeleza jukumu lake kumpokonya Rais Uhuru Kenyatta kura za Mlima Kenya na kwa njia hiyo kumpa ushindi Rais-mteule Ruto dhidi ya kiongozi wa upinzani Raila Odinga.** PICHA I FRANCIS NDERITU

• Na MACHARIA GAITHO

Mteja wa mara ya kwanza katika New Madina Restaurant, eneo la Xiaobei Lu, jiji la Guangzhou, China, atashtuka akifikiri ameingia mkahawa wa 'Little Murang'a', kwenye vichochoro vilivyojaa watu vya eneo la kati la jiji la Nairobi.

Katika baadhi ya misimu, lugha inayosikika kwa wingi ni Kikuyu, kutoka kwa wafanyabiashara wengi waliofika China kununua bidhaa za kuuza Kenya.

Mkahawa huo ni maarufu kwa Wakenya na wageni wengine kutoka Afrika wasiokula chakula cha kigeni. Chakula hapa ni kuku, mchuzi wa nyama ya ng'ombe au kondoo kwa wali au chapati na bei yake ni nafuu sana.

Mkahawa wa New Medina, unaomilikiwa na familia ya raia wa China, ambao ni Waislamu, uko katika jumba la Deng Feng, ambalo lina hoteli, maduka kadhaa ya reja reja na kampuni kadhaa za kusafirisha bidhaa Kenya na nchi nyingine za Afrika Mashariki, Nigeria, Mali, Senegal na nchi nyingine zote za Afrika Magharibi.

Baada ya kula katika mkahawa wa New Madina, wafanyabiashara hao hutembelea maduka kadhaa ya bidhaa za elektroniki eneo la Dashatou, safari ya dakika kumi kwa gari. Akiulizwa bei ya runinga za kisasa, mhudumu wa duka ataonyesha aina kadhaa kutoka Japan, Korea Kusini na aina mpya kutoka China: "Sony, Samsung, Panasonic, Hitachi, Haier, Toshiba, Hisense, Wewe sema..." "Niseme nini?" "Wewe sema".

Mwelekezi anayeandamana na wafanyabiashara hao anawaeleza kwamba "Wewe sema" si aina ya runinga, bali mteja anaulizwa aina anayotaka. Kisha nembo inayofaa inawekwa kwa televisheni yoyote isiyo na jina ambayo imewekwa kwa maonyesho.

Wafanyabiashara hao hununua bidhaa zao, mara nyingi kwa wingi, na kupitia mfumo thabiti. Kampuni za usafirishaji wa bidhaa Kenya zilizo na matawi jijini Guangzhou na vituo vingine vya biashara China, huchukua bidhaa hizo, kuzipakia vyema na kuhakikisha zinasafirishwa kwa meli au ndege.

Mfanyabiashara huchukua bidhaa zake katika mabohari eneo na Eastleigh, Nairobi, au zinasafirishwa moja kwa moja katika duka lake la jumla au reja reja.

## SH1.5BN

Mambo yaliharibika hata zaifi mnamo Agosti 2018 Rais Kenyatta aliposhuhudia moto ukichoma bidhaa haramu za thamani ya zaidi ya Sh1.5 bilioni.

Kampuni za usafirishaji, ambazo nyingi zinamilikiwa na Wasomali kutoka Kenya nchini China, Dubai, Uturuki na kwingine wafanyabiashara wa Kenya wanakoenda kwa wingi, hufanya kazi kwa uwezo na kuaminiana kwa hali ya juu.

Ni vigumu kusikia bidhaa zimepotea, kupelekwa maeneo tofauti na zilikofaa kupelekwa au kubadilishwa. Mara nyingi, wafanyabiashara hulipa baada ya kupokea bidhaa zao. Muujiza huu wa kushughulikia bidhaa pia huwa katika forodha. Bidhaa humfikia mwenyewe jinsi zilivyopakiwa, bila kufunguliwa na maafisa wa forodha na ushuru kukaguliwa. Baada ya bidhaa kufika, mteja hulipa gharama ya usafirishaji, bila kupewa risiti za ushuru wa uingizaji bidhaa au stakabadhi za kuonyesha zimechunguzwa kubaini viwango vya ubora.

Karibu kwa uchumi wa Nyamakima.

Eneo hili la biashara za 'mahasla', Nairobi, katikati ya barabara za River Road na Kirinyaga, limekuwa likivuma kinachojulikana kama moyo wa kibiashara wa Mlima Kenya. Lilitekeleza jukumu lake kumpokonya Rais Uhuru Kenyatta kura za Mlima Kenya na kwa njia hiyo kumpa ushindi Rais-mteule William Ruto dhidi ya kiongozi wa upinzani Raila Odinga.

Ni hatua ya serikali ya kuzima ulanguzi wa bidhaa kuanzia 2017 ambayo Naibu Rais William Ruto alitumia kueneza propaganda na kumfanya Rais Kenyatta adui mkuu wa biashara za jamii

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media






Biashara katika eneo la Nyamakima Septemba 7. PICHA | FRANCIS NDERITU

ya Wakikuyu.

Kampeni ya Ruto ya walalahoi dhidi ya matajiri, na sera yake ya kuinua uchumi kuanzia chini, ilifurahisha wafanyabiashara na mafundi wadogo ambao walikuwa wameathiriwa na kudorora kwa uchumi, ambako Ruto alilaumu Rais Kenyatta, licha ya ukweli kwamba ulisababishwa na masuala kadhaa ambayo hangeweza kudhibiti kama vile janga la Covid-19, kupanda kwa bei za mafuta ulimwenguni na uvamizi wa Urusi nchini Ukraine.

Afisa Mkuu Mtendaji wa Muungano wa Wafanyabiashara Wadogo, Sammy Karanja, anasema mambo yaliharibika hata zaifi mnamo Agosti 2018 Rais Kenyatta aliposhuhudia moto ukichoma bidhaa haramu za thamani ya zaidi ya Sh1.5 bilioni.

Wakati huo, Rais aliapa kuendelea kufanya hivyo akisema hatua hiyo ilinuiwa kulinda viwanda vya Kenya na watumiaji bidhaa lakini akatumbukia katika propaganda ambayo Ruto na washirika wake kutoka Mlima Kenya walikuwa wakieneza.

Naibu Rais aliendelea kumshambulia Rais kwa kusukuma Wakenya wa kawaida kwa Fuliza, mojawapo ya mikopo inayopatiaka kupitia kwa simu. Sasa inaibuka kuwa kunyooshea kidole cha lawama bidhaa inayohusishwa na Benki ya NCBA ambayo umiliki wake pia unahusishwa na familia ya rais, kulikuwa makusudi na kulilenga vita vya kibiashara.

Hata hivyo, swali ni: Kwa nini vita vya dhidi ya ulanguzi na ukwepaji ushuru viligeuzwa kuwa suala la Wakikuyu?

Wingi wao katika mkahawa wa New Madina unaelezea sababu. Kulingana na Karanja, idadi kubwa zaidi ya wafanyabiashara wanaoenda China, Dubai na Uturuki wanatoka Mlima Kenya.

Huo ni mtindo wa tangu miaka ya 2000, wafanyabiashara wa eneo hilo walipofanya ziara zao za kwanza China, wakaona nafasi na wakaanza kualika jamaa na marafiki na kusababisha kuongezeka kwa safari za kununua bidhaa.

Eneo la Nyamakima sasa lina mamia ya maduka ya rejareja yanayouza bidhaa za elektroniki, bafu, vifaa vya jikoni, taa, mazulia, majenereta, vipuri vya magari, viatu, simu za mkononi na karibu kila kitu.

Eneo hilo, ambalo sasa limepanuka zaidi hadi nje ya kilichokuwa kituo cha matatu cha Nyamakima, pia linasambaza bidhaa hadi maeneo mengine ya Kenya.

Bidhaa za bei nafuu zinazouzwa na wachuuzi katika misongamano ya magari Nairobi au kwenye baa na masoko jijini hutoka Nyamakima. Vile vile, bidhaa zingine bora katika majumba ya kifahari ya biashara hutoka eneo hilo. Hili linaibua suala lingine. Sio bidhaa zote kutoka Nyamakima ambazo ni duni, bandia au za bei rahisi.

Mtu anaweza kupata bidhaa bora na halisi kutoka Ulaya na Amerika na pia kwa bei sawa na ya bidhaa kutoka China. Mtu pia anaweza kupata zile bandia za "Wewe sema" au zilizo na nembo inayofanana na zile halisi, kwa mfano Sumsang, badala ya Samsung.

Naam, kuna masuala kuhusiana na ukwepaji kulipa ushuru na ubora. Kulingana na Karanja, shirika lake haliungi mkono ukwepaji ushuru au kuingiza bidhaa bandia lakini wanataka ufahamu na ukweli katika utekelezaji.

Anasema hata wakati wanaoleta bidhaa kutoka nje wakikosa kulipa ushuru moja kwa moja kwa Shirika la Ushuru Kenya, ushuru huo unawekwa chini ya ada za usafirishaji zinazolipwa maajenti wa kampuni. Badala ya kutoza ushuru bidhaa binafsi kwa kutegemea thamani yake, KRA hutoza ushuru kwa kutegemea wingi wa bidhaa. Shida, anasema, ni wakati KRA inapoongeza ada bila ilani kutoka Sh1.3 milioni hadi Sh2.2 milioni kwa kontena ya futi 20 ilivyofanyika mwaka jana. Au wakati mfanyabiashara analipia Sh1 milioni na wiki inayofuata mwingine anatozwa Sh1.8 milioni kwa shehena sawa.

**Katika soko la China, unapata unacholipia. Unaweza kupata bidhaa za ubora wa hali ya juu na zilizo halali kutoka Ulaya na Amerika, na pia upate bidhaa sawa na hizo zilizoundwa China kwa bei nafuu sana. Unaweza pia kupata nyingine feki zenye chapa zinazokaribiana na zile halali kama vile Sumsang badala ya Samsung.**

Haya ndiyo masuala ambayo chama chake kiliwasilisha kwa Ruto katika mikutano mitatu na akawasikiliza. Sasa ni matumani yake kuwa Ruto ataondoa vikwazo kwa biashara na kuruhusu biashara ndogo kunawiri. Anataka sekta isiyo rasmi ilainishwe ili wahusika waache kuendesha shughuli zao kichinichini na kuchukua nafasi yao katika mazingira ya uchumi.

Hata hivyo, huenda wengi katika sekta hiyo huenda wasikubaliane na maoni yake. Heri wasilipe ushuru kwa serikali, Shirika la Ubora wa Bidhaa Kenya, Wakaguzi wa Baraza la Kaunti au mamlaka yoyote ile.

Hawa ndio watafahamu kwamba kuundwa kwa serikali ya 'hasla' ya Rais Ruto hakutakuwa leseni ya kushiriki ulanguzi na kukwepa kulipa ushuru. Kauli za kampeni ni tofauti na utawala.

# Wakati kuria alipocheza na moto

• Na MACHARIA GAITHO

Aliyekuwa Mbunge wa Gatundu Kusini, Moses Kuria aliongoza kampeni ya kumlaumu Rais Uhuru Kenyatta kwa kuharibu biashara za watu wa Mlima Kenya kupitia misako ya wanaokwepa kulipa ushuru, ulanguzi na bidhaa feki.

Kufikia mwisho wa Aprili 2019, Bw Kuria aliunga mkono hadharani uingizaji nchini wa bidhaa feki, akitaka Waziri wa Biashara, Peter Munya, afutwe kazi baada ya kuweka mikakati ya kuhakikisha ubora wa bidhaa na kuharibu bidhaa feki kutoka China.

Bw Kuria alidai uchumi wa China ulikua kutokana na uwezo wake wa bidhaa bandia. "Napendekeza bidhaa yoyote bandia mbayo haitengenezwi humu nchini. Tutajifunza kutengeneza bidhaa halali baadaye," akasema.

Baadaye Septemba 2021, ilitokea hali sawa na ya mtu kupata ulichotaka. Bw Kuria alikuwa akitumia zulia la stima kutibu hali ya miguu kuganda kifaa hicho kilipoharibika.

*"Napendekeza bidhaa yoyote bandia mbayo haitengenezwi humu nchini. Tutajifunza kutengeneza bidhaa halali baadaye."*

Kuria alisema zulia hilo lililipuka moto na kuchoma miguu yake vibaya. Matibabu katika hospitali nzuri Kenya na India hayakumsaidia, na hakupona hadi Februari mwaka huu kufuatia upasuaji nchini Dubai.

Oktoba mwaka jana, akiwa bado amelazwa katika hospitali Nairobi, Bw Kuria alitoa ushahidi mbele ya Kamati ya Bunge iliyokuwa ikichunguza kampuni ya Ceragem Ltd, inayosambaza kifaa kilichomchoma miguu.

Alilaumu kampuni hiyo kwa kuuza bidhaa hatari ambazo hazijafikia viwango vya ubora vya Shirika la Ubora wa Bidhaa Kenya (KBS), na kutisha kuishtaki kwa masaibu aliyopitia.

ePaper Copy Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Kenya

MNARA WA MAMLAKA

# RAIS RUTO TAYARI KUCHAPA KAZI

*Kutoka muuzaji wa kuku hadi kuwa Amiri-Jeshi Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi Kenya, Ruto amejionea mengi. Baada ya kumaliza mihula miwili akiwa Naibu Rais, na maisha yake yote ya kazi akiwa karibu na mamlaka, inawezekana tayari Dkt Ruto anaelewa vyema anachotaka kufanya na jinsi anavyotaka kukifanya.*

● Na MACHARIA GAITHO

Atakapokuwa akichagua nguo za kuvaa kwa siku muhimu katika maisha yake, William Samoei Ruto, hatakuwa akiwaza tu safari yake ya ufanisi ya mwanakijiji aliyetembea bila viatu hadi kuwa Rais wa Kenya na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi, bali pia anachohitaji kufanya kuunda ofisi hiyo katika sura yake mwenyewe.

Baada ya kumaliza mihula miwili akiwa Naibu Rais, na maisha yake yote ya kazi akiwa karibu na mamlaka, inawezekana tayari Dkt Ruto anaelewa vyema anachotaka kufanya na jinsi anavyotaka kukifanya.

Huenda atakuwa ameangalia marais wanne waliomtangulia - Jomo Kenyatta (1963-1978), Daniel arap Moi (1978-2002), Mwai Kibaki (2002-2013) na Uhuru Kenyatta (2013-2022) - na kutwaa mafunzo kutoka kwa tawala hizo.

Wote walikuwa walikuwa na bidii ya kutafuta mamlaka, na walipoingia ofisini, walijikinga dhidi ya vitisho vya aina yoyote. Walitawala nyakati tofauti na chini ya katiba na mazingira tofauti ya kisiasa, kutoka utawala wa kidkteta wa chama kimoja wa Jomo na Moi hadi utawala wa demokrasia wenye kelele na usio na mpangilio wa Kibaki na Uhuru.

Bado kuna mengi ya kusoma, na kitu kimoja kinachojitokeza wazi ni kuwa kupanda ngazi kwa Ruto kunaendeleza uthibiti wa Wakalenjin na Wakikuyu ambao huenda wakachukiwa tena na jamii zingine. Kuna mengi yanayolingana kati ya kupanda ngazi kwake na mtangulizi wake wa pekee aliyemtaja kamuwa mlezi wake, Daniel arap Moi.

Jambo moja linalojitokeza wazi ni kiongozi Mkalenjin kuwa naibu wa rais mkikuyu, kuvumilia kudhulumiwa na hatimaye kuibuka mshindi.

Hadithi za Moi na Ruto ni masimulizi ya vuta-nikuvute ya namlaka kati ya Wakikuyu na Wakalenjin. Watu kutoka jamii hizi mbili wamekuwa wakiungana mkono kuingia mamlakani huku wakitenga jamii zingine, na wakati huo huo kuzua ugomvi ambao hatimaye wanauweka kando ili kupokezana hatamu za uongozi.

Katika miaka ya mwanzo ya uhuru, Jomo Kenyatta alimhitaji Moi kumsaidia kumzima Oginga Odinga, aliyekuwa tumaini la Waluo kisiasa. Oginga alikuwa amezimwa Jomo alipokufa 1978, na tisho pekee lililobaki kwa Moi kuingia mamlakani kundi lililofahamika kama 'Kiambu Mafia'.

Moi alikuwa mwerevu sana kuwa na marafiki Wakikuyu, wakiongozwa na Charles Njonjo, kurahisisha safari yake ya kuingia Ikulu.

Alipoingia mamlakani alitumia wakuu wa serikali na vikosi vya usalama waliodhibitiwa na Njonjo kuzima watu maarufu waliobaki katika utawala wa Kenyatta - Njoroge Mungai, Mbiyu Koinange, Njenga Karume na Kihika Kimani – ambao bado waliamini alikuwa wingu linalopita.

Baada ya kutimiza hayo, Moi alimgeukia Njonjo, na Kibaki na Wakikuyu wengine wote aliohisi wangekuwa wapinzani wake huku akiunda kundi lake la 'Kalenjin Mafia' katika nyanja za kisiasa, uchumi, usimamizi na usalama.

Kutoka siku yake ya kwanza ya utawala wake, Moi alijionyesha kama mtakatifu, kiongozi mbeba Biblia aliyechukia ufisadi na ambaye hakuwa na tamaa ya mali. Mmoja wa misemo yake tangu wakati huo ni kwamba kitanda cha dhahabu hakiwezi kununua usingizi.

Lakini muda si mrefu ilibainika kuwa mojawapo la mambo muhimu kwake lilikuwa kulimbikiza utajiri mwingi kushinda wapinzani wake katika serikali iliyotangulia.

Alipora mali ya umma kwa pupa na wakati huo huo kubomoa ngome za kiuchumi za wapinzani wake.

Ruto si Moi. Amesoma zaidi, amejua mengi na anatawala katika kipindi tofauti kabisa cha katiba inayozima udikteta na matumizi mabaya ya mamlaka.

Hata hivyo, anajua kuwa rais akitaka anaweza kutumia ofisi yake kujitajirisha. Kauli ya kampeni yake ya Serikali Kutekwa Nyara ilikuwa mbinu ya kujitetea dhidi ya madai ya ufisadi, akiwaanyooshea kidole cha lawama waliomlaumu. Lakini inawezekana ilitokana na mambo aliyoshuhudia mwenyewe.

Iwapo Ruto atatimiza ahadi yake ya kuunda tume ya kuchunguza waliopora mali ya serikali, atakuwa amelenga himaya kubwa ya biashara za familia ya Kenyatta, lakini inasubiriwa kuona iwapo atafanya hivyo.


Ruto, ambaye ni mchapa kazi, asiyekunywa pombe, mbeba-biblia, sawa na Moi, pia alitegemea kura za Wakikuyu, kama si viongozi Wakikuyu, kuingia mamlakani. Yeye pia ameingia mamlakani na Naibu Rais Mkikuyu, ingawa ana wafuasi wake mwenyewe eneo la Mlima Kenya, kwa hivyo si mateka wa Rigathi Gachagua.

Huenda hatakuwa na hofu aliyokuwa nayo Moi, lakini uhusiano wao utategemea Naibu Rais kufanya kazi yake bila kuonyesha tamaa ya uongozi.

Hata hivyo, apende asipende, akiwa Naibu Rais, Gachagua atakuwa tegemeo la kisiasa la Mlima Kenya wakati wa kutafuta mrithi wa Ruto.

Gachagua akiruhsu hili kumuingia akilini, huenda Ruto akalazimika kutumia mikakati aliyotumia Moi kumzima naibu wake ambaye anafikiri ana kura nyingi.

Musalia Mudavadi, ambaye ameahidiwa cheo cha Mkuu wa Mawaziri na wengine wengi, watakuwa wakisubiri fursa kama hiyo itokee ili wanufaike.



ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Kenya

SIASA ZA MPITO

# KINYANG'ANYIRO CHA VYEO

*Mabadiliko ya serikali yanaweza kuathiri kazi za watumishi wa umma wanaoteuliwa kisiasa.Uteuzi wa maafisa wa serikali huwa vuta-nikute ambapo ushawishi serikalini hupimana nguvu. Serikali ya kwanza ya Jubilee ilitumia mtindo ambao haukuzingatia wala kujali maslahi ya baadhi ya Wakenya*

• Na JAINDI KISERO

JUMANNE ya Mei 2019, bodi ya Mamlaka ya Ushuru Kenya (KRA) chini yaikiongozwa mwenyekiti wake, Edward arap Sambili, ilifanya kikao maalumu. Ajenda kuu ya mkutano huo ilikuwa kumpa Afisa Mkuu Mtendaji (CEO), John Njiraini, likizo ya mwisho kabla ya kustaafu na kumteua David Kiprop Yego kuwa Afisa Mkuu Mtendaji mpya. Agizo la kuandaa mkutano huo lilitoka kwa Naibu Rais William Ruto.

Katika hatua wazi ya kuonyeshana ubabe, Ijumaa wiki hiyo Rais Uhuru Kenyatta alichapisha taarifa maalumu katika gazeti rasmi la serikali kuvunjilia mbali bodi nzima ya KRA. Mwenyekiti wake, Edward Sambili, alibanduliwa na nafasi yake ilichukuliwa na aliyekuwa Mkuu wa Utumishi wa Umma Francis Muthaura.

Rais Kenyatta aliagiza Bw Njiraini aendelee kuongoza KRA kwa miezi kadhaa hadi Afisa Mkuu Mtendaji wa sasa, James Githii Mburu, alipoteuliwa.

Chini ya makubaliano ya kabla ya uchaguzi kati ya Rais Kenyatta na Dkt Ruto, Hazina Kuu ya Kitaifa na idara nyingine zilizo chini yake zilifaa kusimamiwa na vigogo kutoka eneo la Bonde la Ufa walioteuliwa na Dkt Ruto.

Washirika wa Dkt Ruto walikuwa wakilalamika kuwa, mbali na aliyekuwa Waziri wa Fedha, Henry Rotich, idara muhimu – KRA na Benki Kikuu ya Kenya – zilisimamiwa na watu walioteuliwa na Rais Kenyatta. Kiprop Yego hakupata kazi ya KRA.

Kisa hicho kinaonyesha jinsi mabadiliko ya serikali yanaweza kuathiri kazi za watumishi wa umma wanaoteuliwa kisiasa.

Uteuzi wa maafisa wa serikali huwa vuta-nikute ambapo ushawishi serikalini hupimana nguvu. Serikali ya kwanza ya Jubilee ilitumia mtindo ambao haukuzingatia wala kujali maslahi ya baadhi ya Wakenya.

Uteuzi wa maafisa wa serikali kwa misingi ya kisiasa haukuanza na Jubilee. Lakini Uhuru na Ruto walikiuka mipaka kwa kutumia mtindo ambao haukuwa umeandikwa popote ambapo vyeo vikuu katika wizara na mashirika ya serikali viligawanywa kwa watu wa jamii hizo mbili waliotoa msaada mkubwa kwenye kampeni za uchaguzi za chama hicho.

Matokeo ya mfumo huo ni kwamba serikali ya Jubilee ilijipata na watumishi wa umma waliotumia jino na ukucha kukabiliana na mageuzi yoyote yaliyotishia ubabe wao.

Nchi ilijipata na watumishi wa umma wasio na nidhamu, madeni yalizonga mashirika ya umma, ufisadi ulikolea, vyuo vikuu viliishiwa na pesa na maafisa wakuu serikalini wakalipwa mishahara minono huku wadogo wao wakilipwa mishahara duni.




Mojawapo la mambo ya kuzingatia katika serikali inayoingia ya Ruto ni idadi kubwa ya viongozi wengi waliochaguliwa ambao wanaandamwa na kesi mbaya za ufisadi.

Rais-mteule William Ruto anachukua serikali ambapo kandarasi zinatolewa kwa bei za juu zaidi kwa wakandarasi walio ndani ya serikali, ambapo wenye viwanda wakuu walio na ushawishi serikalini hawalipi ushuru wala bili za stima, na ambapo mapato yamepungua na madeni ni hali kawaida.

Ushahidi wa yote haya yote ni kesi ambazo Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, Noordin Haji, amekuwa akipeleka kortini dhidi ya watumishi wa serikali wanaoandamwa na kashfa za ufisadi.

Kuanzia Bodi ya Kitaifa ya Nafaka na Mazao (NCPB), Shirika la Umeme Kenya (Kenya Power), Shirika la Ubora wa Bidhaa Kenya (Kebs), Bima ya Kitaifa ya Afya (NHIF), Wizara ya Afya, ama Huduma ya Taifa kwa Vijana (NYS) na kashfa ya mabilionea wa Covid – 19, mawaziri na wakuu wa mashirika ya serikali wanatoa kandarasi kiholela kwa manufaa yao binafsi.

Miradi mikubwa ya miundomsingi iliyoanzishwa kwa nia njema imegeuzwa vyombo vya wanasiasa kupokea hongo kutoka kwa wanakandarasi.

Bajetiza za miradi zinaongezwa na mikataba ya kandarasi kubadilishwa mara kwa mara ili kuwezesha wakuu serikalini kuvuna mabilioni ya pesa kutokana na miradi hiyo.

Mojawapo la mambo ya kuzingatia katika serikali inayoingia ya Ruto ni idadi kubwa ya viongozi wengi waliochaguliwa ambao wanaandamwa na kesi mbaya za ufisadi.

Kenya ya sasa inaendeleza uchumi kilaghai, maarufu kama 'wash wash'- ambapo wafanyabiashara walaghai wanafanya biashara ya bidhaa ghushi, mihadarati, silaha na pesa za bandia.

Kila mara tulisikia maafisa wa polisi wamenasa fedha bandia, mitandao ya magendo ya dhahabu au kukamatwa kwa mihuri feki ya KRA ikiingizwa humu nchini.

Lakini kinachoshtua ni kwamba huwa kuna uhusiano wa karibu kati ya mitandao hiyo ya wahalifu na vigogo wa kisiasa.

Miaka michache iliyopita, aliyekuwa waziri, Rashid Echesa, alikabiliwa na sakata ya kutumia ushawishi wake wa kisiasa kulaghai wafanyabiashara wa kigeni kuwa angewasaidia kupata kandarasi ya silaha kutoka kwa serikali.

Mwaka jana, ilikuwa ni kundi la wafanyabiashara wa dhahabu mjini Dubai wakidai kutapeliwa na kundi la walaghai wanaoshirikiana na wanasiasa kwenye kisa kilichoonyesha jinsi ufisadi hapa nchini unavyoendeshwa kwa ushirikiano wa wakuu wa serikali na magenge ya wahalifu.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Kenya

USAKAJI WA KIGOGO MPYA

# JE, RAILA AMEINUA MIKONO?

*Masuali yameibuka kuhusu ni nani atakayechukua usukani wa jukumu la uongozi lililotekelezwa na aliyekuwa waziri mkuu katika jamii ya Waluo eneo la Nyanza, kama mwangalizi wa watu na kiongozi wa chama iwapo atajiondoa kwenye ulingo wa siasa.*

- Na OSCAR OBONYO

Anapowaza kuhusu hatua yake mpya kisiasa baada ya jaribio lake la tano la kuwa rais kuambulia patupu, minong'ono kuhusu mrithi wa Raila Odinga imeshika kasi haraka katika ngome yake.

Je kuna mpango wowote wa urithi katika Azimio la Umoja-One Kenya na Orange Democratic Movement (ODM) endapo Raila ataondoka kwenye uga wa siasa mwaka huu? Je, vipi kuhusu ngome yake ya nyumbani eneo la Nyanza na katika familia kuu ya Odinga?

Kupitia taarifa iliyotumwa Jumatatu, Septemba 5, punde tu baada ya Mahakama ya Upeo kufutilia mbali kesi yake ya kupinga ushindi wa William Ruto, kinara huyo wa Azimio alisema amekubali uamuzi wa korti lakini akaapa kuendelea kupigania uwajibikaji: "Tutawasiliana hivi karibuni kuhusu mipango yetu ya kuendelea kupigania uwazi, uwajibikaji na demokrasia."

Kulingana na duru za karibu na Raila, kustaafu kisiasa hakupo kabisa kwenye mawazo yake. Ndoto yake ya kushinda urais huenda imedidimia lakini kiongozi huyo wa ODM ana mshawasha mkubwa wa kutetea maslahi ya Wakenya.


Ripoti zinasema kuwa ana wasiwasi kuhusu uwezekano wa hatua zilizofanikishwa kidemokrasia kufikia sasa kuhujumiwa na utawala mpya wa Ruto. Kwa sababu ya kulinda juhudi hizo pekee, Raila anakwamilia hapo kama mwangalizi wa watu.

Lakini msimamo wake huo umepokewa kwa hisia tofauti. Baadhi ya wandani wake, baada ya kuvunjwa moyo na yaliyotokea, wanamtaka astaafu kisiasa. Kundi hili linamtaka Odinga kuacha wapiga kura "wasio na shukran" kukabiliana na matokeo – iwapo yatakuwepo – ya maamuzi yao. Wanamshauri 'Baba' apumzike na kuishi miaka yake ya uzeeni kwa amani na kujiliwaza na familia yake.

Kwa upande mwingine, wazo la kustaafu kwa Raila halikubaliki kabisa kwa wanasiasa ambao kwa miaka mingi wamemtumia kuendelea kudumu kisiasa. Sawa na baba yake, aliyejivunia uungwaji mkono wa dhati usio na kifani miongoni mwa jamii ya Waluo katika miaka ya 1970 hadi 1994, Raila anafurahia ufuasi sugu katika eneo la Luo Nyanza, ambako wengi wamemtumia kupanda ngazi za mamlaka.

Kwa karibu karne tatu, Raila ametanda katika jukwaa la kisiasa nchini Kenya kama jitu. Kushindwa kwake katika uchaguzi wa urais tayari kuna athari kuu kwa sababu kumefanya baadhi ya wafuasi wahamie kwa Ruto na kuondoka kwake kutazidi tu kuzorotesha hali zaidi kwa kuacha wazi ngome zake kote nchini kunyakuliwa na mahasimu wake na kudidimiza umaarufu wake.

Katika Azimio, Raila alikuwa wa kwanza tu miongoni mwa vinara 20 wenye hadhi sawa kwa msingi kwamba alikuwa mgombea urais, hadhi ambayo huenda ikabadilika kwa sababu sasa chaguzi zimekamilika. Kiongozi wa chama cha Wiper, Kalonzo Musyoka, tayari ameapa kugombea wadhifa huo wa juu 2027.



Katika ngome ya Raila, Luo Nyanza, chaguzi za ugavana zilishindaniwa vikali, sababu moja ikiwa kwamba zilichukuliwa kama mikakati thabiti kisiasa ya kujiandaa kumrithi Raila. Katika Kaunti ya Homa Bay, kwa mfano, aliyekuwa gavana wa Nairobi, Evans Kidero, alijitokeza kwa kishindo ambapo hata baada ya kutembwa katika uteuzi wa chama cha ODM, alifanya kampeni kali na kushindwa kwa kura chache tu na Gladys Wanga.

Wanga alipigiwa debe na Raila kwa sababu wazi zinazohusu kwa kiasi fulani uhasama wa tangu jadi kisiasa kati ya Nyanza ya Kati na Nyanza Kusini, ambao katika miaka ya 1960 ulisababisha ushindani mkali kati ya Jaramogi Oginga Odinga na Tom Mboya.

Nyanza ya Kati inajumuisha Kaunti za Siaya na Kisumu ilhali Nyanza Kusini ina kaunti za Migori na Homa Bay. Kidero, ambaye uhusiano wake na Raila si moto si baridi, aghalabu amekuwa – kikweli ama kimakosa - akihusishwa na njama zinazolenga kumhujumu Raila au kumlazimu kustaafu kisiasa.

Na wakati ambao kiongozi wa chama cha Chungwa amekuwa akijitahidi kudumisha umoja wa Luo Nyanza, Kidero ameonekana kujipanga kimya kimya na taratibu kuibuka kinara wa Nyanza Kusini sawa tu na jinsi marehemu Tom Mboya wa Nyanza Kusini alivyomenyana na baba ya Raila, Jaramogi wa eneo la Kati. Isitoshe, Kidero amemuoa bintiye marehemu Mboya.

Katika eneo la Siaya, nyumbani kwa Odinga, wakili James Orengo alichaguliwa gavana akiungwa mkono pakubwa na Raila, hali inayomweka kifua mbele miongoni mwa wapinzani wake katika kinyang'anyiro cha kumrithi Raila. Aidha, Raila anawapendelea wanasiasa wenye historia ya mageuzi, hasa walioshirikiana naye tangu mwanzo katika miaka ya 1980. Gavana wa Kisumu, Profesa Anyang' Nyong'o, yupo katika kitengo hiki.

Katika siasa za Nyanza, hata hivyo, uongozi haupokezwi au kukabidhiwa hivi tu. Unapiganiwa – wakati mwingine kikatili. Hivi ndivyo ilivyokuwa kati ya Mboya na Jaramogi katika miaka ya 1960, na Raila na Orengo mnamo 1994. Orengo, aliyekuwa wakili na msiri wa Jaramogi, alikuwa chaguo la mzee huyo. Lakini Raila alikula njama na kumshinda Orengo katika makabiliano makali kwenye ngome ya nyumbani iliyosababisha Raila, aliyekuwa kijana wakati huo, kutema chama cha Ford-Kenya na kuhamia chama kipya kilichobuniwa cha National Development Party (NDP).

Raila vilevile aliwabwaga kwa kutumia ujanja wapinzani wengine wakiwemo Nyong'o na Shem Ochuodho, na akaweza kunyakua uungwaji mkono eneo hilo.

Katika kiwango cha familia, ndugu mkubwa wa Raila, Oburu Oginga na dada yake mdogo, Ruth Odinga, walichaguliwa katika chaguzi za Agosti 9 kama Seneta wa Siaya na Mwakilishi Mwanamke Kaunti ya Kisumu, wameorodheshwa miongoni mwa viongozi wanaoweza kumrithi.

Maeneo mengine yanayomvutia Raila ni Magharibi mwa Kenya, ambapo Azimio ilipata magavana wanne miongoni mwa watano (Busia, Vihiga, Kakamega na Trans Nzoia), na eneo la Pwani, ambalo linazidi kuvamiwa kisiasa na Ruto. Kisadfa, magavana wanaoondoka, Wycliffe Oparanya (Kakamega) na Hassan Joho (Mombasa) ni manaibu viongozi wa Raila katika ODM lakini hakujatajwa chochote kuhusu mpango wa urithi.

Baada ya kufumaniwa ghafla bin vuu, Raila, aliyeamini angeibuka mshindi wa urais, huenda akaamua kushikilia siasa kwa muda zaidi ili aimarishe ngome zake kisiasa na kulinda mafanikio ya kidemokrasia yaliyopatikana kufikia sasa kabla ya kustaafu.

Nation Media Group "ePaper Copy"

kurunzi ya Kenya

■ ETI ODINGA NANI? WAMEKATAA KUFUATA MKONDO

# UASI KATIKA ENEO LA RARIEDA

*Eneobunge hili, lililokatwa kutoka sehemu kubwa ya Bondo mnamo 1988, ndicho kitovu cha uasi dhidi ya ufalme wa Odinga kisiasa eneo la Nyanza.*

● Na OSCAR OBONYO

Alipowania urais kwa mara ya kwanza miaka 24 iliyopita, Raila Amolo Odinga alikabiliwa na uasi kutoka ngome yake ya nyumbani Nyanza. Wakati huo, uasi uliongozwa na Mbunge wa Rarieda, Achieng' Oneko. Tangu wakati huo, wanasiasa wa Rarieda wamekuwa kero kuu kwa Odinga.

Katika chaguzi zilizokamilika majuzi, Eliud Owalo - mwanasiasa wa Nairobi kutoka Rarieda – ni miongoni mwa waliofungua milango ya kuingiliwa kwa ngome ya Odinga mashinani Luo Nyanza na mpinzani wake mkuu Rais-mteule William Ruto.

Wajibu wa Owalo ni kama njama ya kisiasa kwa kiasi fulani, ikizingatiwa historia ndefu kati ya mwanasiasa huyo na aliyekuwa waziri mkuu. Mtaalamu huyo wa mikakati, aliyehudumu kama msimamizi wa kampeni za urais za Odinga mnamo 2013, ni miongoni mwa vigogo wa Luo Nyanza waliojunga na mrengo wa Ruto miaka mitatu iliyopita, wakati ilipooneka hatari kufanya hivyo.

Katika Luo Nyanza, Owalo na wenzake kutoka Rarieda si wageni kwa uasi wa kisiasa hasa dhidi ya Raila. Yamkini eneobunge la Rarieda, lililokatwa kutoka Bondo mnamo 1988, ndilo kitovu cha uasi dhidi ya himaya ya kisiasa ya Odinga.

Kifo cha mwanzilishi wa chama cha Ford-Kenya na Mbunge wa Bondo, Jaramogi Oginga Odinga, mnamo Januari 20, 1994, kilimuacha Odinga aliyekuwa kijana wakati huo, bila kinga dhidi ya uasi wa kwanza. Alipotofautiana na mrithi wa Jaramogi, Michael Kijana Wamalwa, na kuunda National Party of Kenya (NPK), Oneko aliongoza uasi wa kuhamia chama kipya.

Shujaa wa uhuru, alimwambia wazi Odinga hangemruhusu kuongoza wabunge wa Luo Nyanza kutoka Ford-Kenya kujiunga na NPK: "Nilitumia miaka mingi ya ujana wangu katika siasa nikimpigia debe baba yako na haiwezekani nimfuate mwanawe pia. Wewe – wala si mimi – ndiye unafaa kunifuata," akasisitiza Oneko, ambaye ni miongoni mwa mashujaa sita wa uhuru waliofungwa na serikali ya kikoloni katika gereza la KapenGuria na kuwa maarufu kama "Kapenguria Six."

Pamoja na wengine, Oneko alisombwa na "Tinga" (nembo ya NPK) katika chaguzi zilizofuata za 1997. Nafasi yake ilitwaliwa na George Odeng' Ngure wa NPK. Sawa na baba yake, Lwande Oneko, baadaye alijiunga na siasa kupitia chama ambacho sasa kinaongozwa na Moses Wetang'ula. Alihama mapema mwaka huu na kujiunga na Democratic Action Party-Kenya (DAP-K), kinachohusishwa na Waziri wa Ulinzi, Eugene Wamalwa.



Achieng' Oneko

Tangu hapo kumekuwa na Raphael Tuju, aliyekuwa mbunge wa eneo hilo kati ya 2002 na 2007 na ambaye alitofautiana na Odinga na kuongoza kampeni za 2007 za urais wa Mwai Kibaki eneo la Nyanza. Mnamo 2017, akiwa Katibu Mkuu wa chama cha Jubilee, Tuju alifanikisha azma ya Uhuru ya kuchaguliwa kwa muhula wa pili.

Mrithi wa Tuju 2007, Nicholas Gumbo, anakiri kuwa alianza vyema na Odinga "hadi mambo yalipokwenda mrama nilipoamua kugombea ugavana Siaya." Katika tawala zote mbili – 2017 na mwaka huu – Gumbo anasema alitofautiana na Odinga na akalazimika kuwania kama mgombea huru na kwa chama cha United Democratic Movement (UDM) mtawalia. Aliamua kumfuata Ruto baada ya UDM kujiondoa katika kambi ya Odinga ya Azimio La Umoja – One Kenya. Kwake yeye, ni hali tu ya kupigania nafasi yake kisiasa na anaamini UDM itampa fursa hiyo.

**2017**

Akiwa Katibu Mkuu wa chama cha Jubilee, Tuju alifanikisha azma ya Uhuru Kenyatta ya kuchaguliwa kwa muhula wa pili.

Kuwepo kwa Gumbo, aliyeshindwa kwa kura chache na James Orengo, kunamweka katika njiapanda na muungano wa Azimio. Dhana ni kuwa anatazamiwa kutoa nafasi muhimu ya kuwezesha Kenya Kwanza kupenya katika ngome ya Odinga. Mivutano kati ya Odinga na wanasiasa wa Rarieda huenda ikawa sadfa tu zinazochochewa na maslahi na uhasama wa kisiasa.

Tatizo lingine lisilojulikana kwa watu wasio wa jamii hiyo ni kiburi cha kiukoo na uhasama. Eneobunge asilia la Bondo lilijumuisha koo nne kuu za Waluo kutoka Sakwa, Imbo, Uyoma na Asembo. Joto la kisiasa lilizuka kabla ya chaguzi za 1988, Rais Daniel arap Moi alipopasua eneobunge hilo mara mbili, hatua iliyoaminika kunufaisha wandani wake kisiasa.

Katika mpangilio huo mpya, koo za Sakwa na Imbo zilianguka Bondo, huku Uyoma na Asembo zikienda katika eneo jipya lililoundwa la Rarieda.

Huku kiongozi wa upinzani Jaramogi akijivunia ufuasi sugu eneo la chini la Bondo, hatua ya kuunda Rarieda ilinuiwa kupatia eneo hilo uongozi mbadala na ulio bora. Kwa namna fulani, Rarieda ilikuwa matokeo ya upinzani wa kisiasa dhidi ya familia ya Odinga, na inaonekana wanasiasa wa kizazi hiki wanafuata mkondo huu bila kufahamu.

Kwa miaka mingi, hatua ya kuchukua msimamo imara dhidi ya Odinga kisiasa imekuwa na matokeo yake. Mnamo 2007, kwa mfano, Tuju anasema alilazimika kumsafirisha mama yake Nairobi ili kumuokoa kutokana na vijana wahuni "waliokuwa wakimrushia cheche za matusi kwa Kiluo."

Owalo anaonya kuhusu hatari ya kufuata mkondo. "Naamini huwezi ukapiga hatua maishani iwapo wewe si mtu wa kujaribu mambo yanayohofiwa kuwa hatari. Uwezo wa kufanya maamuzi ni kiungo muhimu cha uongozi, ilhali uongozi huo unahusu kuchukua hatua hatari na kuwa na mikakati ya kujikinga dhidi ya athari hizo," anasema Owalo, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa UDA.

Hata hivyo anaamini dhana ya chuki ya wanasiasa wa Rarieda dhidi ya Raila ni sadfa tu "kwa sababu tofauti hizi si za kijiografia bali za kimsimamo kutokana na hali ya wakati huo."

Hii inaelezea kwa kiasi fulani mkwaruzano wa muda mfupi kati ya Raila na Dkt Otiende Amolo, mbunge wa sasa wa eneo hilo. Mnamo Mei 2021, wakili huyo alionekana kukanyaga kidole cha bosi wake kuhusu Mpango wa Maridhiano (BBI), baada ya kutahadharisha kuhusu vipengee kadhaa na jinsi mchakato huo ulivyokuwa ukitekelezwa.

Chama cha ODM kilimtimua katika Kamati ya Bunge la Kitaifa kuhusu Haki na Masuala ya Sheria alimokuwa naibu mwenyekiti. Nafasi yake ilipewa Mbunge wa Ruaraka, TJ Kajwang.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Habari kwa picha



**Waendeshaji baiskeli wawasha mishumaa wakisubiri mwili wa Suleiman Kangangi katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Eldoret Septemba 6. Kangangi alifia nchini Amerika kutokana na ajali wakati wa mbio za baiskeli za 'Vermo Overland'.** PICHA | JARED NYATAYA



**Waumini wa dhehebu la Hindu wajitahidi kunywa mvinyo kama sadaka kutoka kwa sanamu ya Sweta Bhairav, mungu wa ulinzi, siku ya kwanza ya tamasha hilo mjini Kathmandu Septemba 7.** PICHA | AFP



**Sherehe mjini Eldoret, Kaunti ya Uasin Gihu, baada ya Mahakama ya Upeo kudumisha kutangazwa kwa William Samoei Ruto kuwa Rais-mteule Septemba 5.** PICHA | JARED NYATAYA



**Wafanyakazi wakibeba mchoro katika eneo la kuhifadhi michoro la kanisa la Notre-Dame de Paris viungani mwa jiji la Paris Septemba 6.** PICHA | AFP



**Sehemu ya msitu karibu na mjiji la Hotens, kusini-magharibi mwa Ufaransa, uliochomeka wakati wa mioto ya Landiras. Nchi hiyo imekumbwa na visa vingi vya moto msimu huu wa kiangazi ambapo hekta zaidi ya 30,000 za msitu ziliharibiwa Julai na Agosti.** PICHA | AFP



**Watoto wa wafanyakazi wanaoishi mtaa wa mabanda wakicheza karibu na nyumba zao zilizoingia maji kufuatia mvua kubwa jijini Bangalore, India.** PICHA | AFP

Nation Media Group "ePaper Copy"

Jukwaa La **Vijana**











PICHA ZOTE | KEVIN ODIT

# WAMEVALIA NJUGA MAJI MAKUU

*Huku Kenya ikijitahidi kuvuna rasilimali zake za baharini, wanawake sita wamepokea mafunzo ya uvuvi wa maji makuu, kazi ambayo kufikia sasa imetawaliwa na wanaume*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

NAFASI YA VIJANA

# UNGANISHA NCHI IPATE KUPONA

**SAUTI YA VIJANA** Rais ana jukumu la kujenga umoja wa kitaifa kwa kushirikisha wananchi wote katika kuteua maafisa wa wizara za serika

• NA ERIC NAKHURENYA



MAHAKAMA ya Upeo Jumatatu ilihalalisha uchaguzi wa Dkt William Ruto kuwa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Kenya. Baada ya miezi kadhaa ya kampeni kali, Wakenya sasa wanaweza kurudu kazini na kuendelea na shughuli zao za kila siku ili kukimu familia zao.

Ingawa ni rahisi kusema Wakenya ndio washindi katika chaguzi zilizokamilika majuzi, ambapo amani ilidumishwa katika maeneo mengi, sote tunafaa kuzingatia maneno ya Naibu Jaji Mkuu Philomena Mwilu, kuwa katika kesi, sawa tu na katika ushindani wa kisiasa, ni lazima kutakuwa na mshindi na aliyeshindwa. Swali kuu ni je, serikali mpya inahitajika kufanya nini kujenga nchi yenye umoja ambao utaleta ufanisi kwa Wakenya wote?

Rais ana jukumu la kujenga umoja wa kitaifa kwa kushirikisha wananchi wote katika kuteua maafisa wa wizara za serika. Rais mwenye nia ya kujenga uzalendo wa kweli, hatashindwa kusawazisha uteuzi serikalini unaozingatia asili yetu tofauti, ambayo ndiyo nguvu yetu.

Jukumu la dharura linalomsubiri Rais mpya ni kuteua baraza lake la mawaziri na maafisa wengine wa umma watakaosaidia serikali kutimiza ahadi zake nyingi.

Akiwa na mamlaka ya uteuzi wa maafisa wote wa serikali, Rais anashikilia ufunguo wa kujenga nchi moja ama kuongoza nchi iliyogawanyika kwa miaka mitano ijayo au zaidi.

Ni wazi kuwa hapo awali Wakenya wamelalamikia jinsi teuzi za serikali zilivyoegemea upande fulani, kusheheni ubaguzi wa kikabila na kupendelea jamaa wa familia. Tunasubiri kwa hamu kuona jinsi Dkt William Ruto atakavyoshughulikia jambo hili.

Ni wajibu wa kila kizazi kuanzisha mwelekeo mpya, na wakati huo ulitimia kwa Wakenya kuchagua kati ya uchaguzi wa amani unaoleta ufanisi na vurugu zinazobomoa mafanikio yote yaliyopatikana kwa miaka mingi.

Serikali mpya inachukua usukani wa taifa lenye amani kiasi lakini lililogawanyika sana kisiasa. Hiali hii inahitaji juhudi za dhati za kuponya taifa na kuunda serikali jumuishi. Licha ya kuwepo kwa amani nchini, tunafaa kufahamu kuwa, kufuatia matokeo ya uchaguzi uliokamilika majuzi, nchi iligawanyika katikati. Ipo haja ya kujenga uhusiano wa karibu wa kufanya kazi kati ya serikali za kaunti na serikali kuu.

Serikali kuu inashikilia bajeti kubwa inayohitaji kusambazwa kwa haki na usawa kupitia utekelezaji wa miradi muhimu ya kitaifa. Maeneo ambayo awali yamekosa maendeleo yanafaa kupewa kipaumbele iwapo tunatumai kufungua nafasi zitakazosaidia Wakenya kukabiliana na baadhi ya matatizo sugu kama vile ukosefu wa ajira.

*Je, wewe ni kijana na una ari ya kufanikiwa? Tungependa kusikia kutoka kwako. Tuma maoni na mtazamo wako kuhusu masuala ibuka kupitia: weeklyreview@ke.nationmedia.com*

## WANAVYOSEMA



**Nellie Aoko**
Licha ya kushindwa, Raila Odinga atasalia kuwa shujaa wa nchi hii. Ni rais ambaye Kenya haitawahi kupata. Tunamsherehekea kwa sababu tumefika tulipo kwa sababu yake. Uhuru tunaojivunia leo ni kwa sababu yake.
*— Afisa wa mauzo kidijitali*



**Joan Muhongo**
Chaguzi hufanywa kwa utawala bora. Ingawa Raila na Ruto wana mawazo tofauti kuhusu jinsi ya kuendesha taifa, wanafaa kutekeleza majukumu yao katika ujenzi wa taifa. Tunahitaji kuimarisha maslahi ya Wakenya.
*— Mtaalam wa saikolojia*



**Mendy Hameda**
Jitihadi zako za kutafuta demokrasia zinawatia moyo Wakenya wote. Juhudi za kupigania utawala bora hazikomi kwa matokeo ya uchaguzi lakini kwako kuendelea kupigania haki za binadamu. Ni matumaini yangu kuwa utazidi kuhamasisha taifa hili.
*— Mwanafunzi*



**Levi Lemayian**
Raila Odinga ni kiongozi mzuri ambaye amepigania demokrasia yetu. Wakati umefika kwake kusimama imara na kufanya kazi pamoja na Rais-mteule William Ruto. Kama kiongozi wa upinzani, anaweza kuhakikisha serikali inawahudumia Wakenya ipasavyo.
*— Mpiga picha*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

KAULI YANGU



# KUHAKIKISHA KAZI YAKO IMEFANYWA

**Wafanyakazi katika biashara:** Uajiri wa wafanyakazi kwa kuzingatia ujuzi wao ndio mtindo unaopendelewa siku hizi. Ndio, ni vizuri kunawiri katika masomo, lakini siku hizi haitoshi kuwa na digrii au diploma pekee.

MFANYABIASHARA yeyote anafaa kuwa na ufahamu kuhusu namna ya kuajiri wafanyakazi wenye maarifa yatakayopanua biashara yake.

Huu ndio ukweli na haujaongozwa na hisia bali unazingatia mantiki na uhalisia wa mambo nyakati hizi.

Wafanyabiashara wengi hutazama biashara zao zikiporomoka kwa sababu waliajiri watu wa familia zao, na marafiki, kuwasaidia kuziendesha.

Hali hii huchangiwa na dhana potovu kwamba watu waaminifu zaidi ni wa familia na marafiki.

Utaratibu wa kawaida wa kuajiri wafanyakazi huanza kwa uwasilishaji wa wasifu (CV) na barua ya maombi ya kazi. Hii ndiyo njia ya haraka ya kuwapata watu wanaofaaa kuhudhuria mahojiano ya kazi.

Inachuja na kukuacha na watu bora wanaoelewa kazi fulani. Hii ni hatua nzuri.

Hata hivyo, jinsi ambavyo utapiga hatua inayofuata ni muhimu katika kuamua aina ya kundi la watu ambao ungetaka kufanya kazi nao.

Richard Brandson, katika makala yake, anaelezea mikakati ya kubaini sifa na tabia za wafanyakazi watakaoajiriwa.

Anasisitiza kuhusu haja ya kuajiri watu ambao wanajali watu wengine kwa kuheshimu haki zao za kibinadamu. Brandson anasema kuna haja ya kuajiri watu wenye ujuzi ili kazi husika iweze kufanyika vizuri.

Anawahimiza wafanyabiashara kuwa na ujasiri na wasiwaandame kwa karibu wafanyakazi wao bali wawaache wafanye kazi zao katika mazingira huru.

Utaratibu huu mpya wa idara za uajiri unaoegemea uzingativu wa ujuzi, unapata umaarufu miongoni mwa wafanyabiashara.

Hii ni kwa sababu ni njia bora ya kuwezesha biashara zao kukua na kufanikiwa.

Ni mbinu ya kuchuja na kuajiri wafanyakazi kwa kuzingatia ujuzi, talanta na maarifa waliyo nayo wala si viwango vya masomo.

Mbinu hiyo ya uajiri pia inazingatia tabia za mtu, ujuzi na hamu ya kazi kwani itawawezesha wafanyabiashara kuajiri wafanyakazi bora.

**Bila kuzingatia umri au cheo chako kazini, jiunge na wengine na ujisajili kwa mafunzo ya ujuzi katika majukwaa kama vile "LinkedIn leaning", "Google dijital skills for Africa", "Trace Academia" na "Cousera"**

Uajiri wa wafanyakazi kwa kuzingatia ujuzi wao ndio mtindo unaopendelewa siku hizi. Ndio, ni vizuri kunawiri katika masomo yako, lakini siku hizi haitoshi kuwa na digrii au diploma pekee.

Unahitaji ujuzi wa ziada ili uweze kupata kazi na kudumu katika kazi hiyo. Huu ndio wakati ambao watu wenye umri mdogo wananawiri kimaisha. Nawahakikishia kuwa huu ndio wakati bora kwa watu hao.

Kila kitu kiko mitandaoni; unahitaji tu kujua kile ambacho unataka, mahala pa kukipata na namna ya kukitumia maishani ili kufikia malengo yako.

Kwa hivyo, bila kuzingatia umri au cheo chako kazini, jiunge na wengine na ujisajili kwa mafunzo ya ujuzi katika majukwaa kama vile "LinkedIn leaning", "Google dijital skills for Africa", "Trace Academia" na "Cousera" ambayo hutoa mafunzo bila malipo kupitia simu yako.

Utasoma kupitia simu yako mikononi na unaweza kuinua kazi yako hadi hatua nyingine.

*Josephine Wanja, Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Black Dot Limited.*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

WARAKA KUTOKA MAJI MAKUU

# BAHARI YA UVUVI YAPATA WAGENI

**WASICHA PIA HUWINDA SAMAKI:** Mjini Mombasa, sio kazi kama kawaida. Wanawake sita wamegeuza majukumu ya jadi ya kijinsia na kujitosa katika uvuvi wa maji makuu ambao umetewaliwa na wanaume.

• Na WINNIE ATIENO

Ni asubuhi tulivu yenye upepo katika kiwanda cha Samaki cha Liwatoni, bandari ya kwanza ya Uvuvi Kenya, Kaunti ya Mombasa, iliyogharimu Sh318 milioni.

Wanawake sita wakiabiri 'The Jonas', mashua ya kuvua samaki katika bahari kuu, wimbi kali linavuma katika Bahari Hindi. Wanatazama maji yanayowazunguka, wakifikiria kinachowasubiri mbele yao - siku kumi za mafunzo kuhusu uvuvi katika bahari kuu.

Wakiwa na umri wa kati ya miaka 23 na 25, hawa ndio wanawake wa kwanza kuhitimu mafunzo ya uvuvi katika bahari kuu Kenya. Awali, walifunzwa uvuvi katika Huduma ya Uvuvi Kenya na baadaye wakatumwa katika Taasisi ya Utafiti wa Baharini na Uvuvi Kenya (KMFRI), ambako walifunzwa kutambua samaki, upimaji, kuchagua na jinsi ya kuvua aina tofauti.

Baadaye walijiunga na chuo cha Maritime Academy kusomea ubaharia. Wanawake hao sita wamepindua majukumu ya kitamaduni na kijinsia kuingia katika ulimwengu wa uvuvi katika bahari kuu unaotawaliwa na wanaume.

Fatma Abdalla, 24, alikuwa akifanya kazi kama mpokeaji wageni katika hospitali moja ya kibinafsi Kaunti ya Kwale alipoona tangazo kutoka kwa serikali la kusajili vijana walio na umri wa kati ya miaka 18 na 35 kufunzwa uvuvi. Msichana huyo kutoka Kisiwa cha Wasini aliamua kujaribu.

"Ninalenga Bandari ya Uvuvi ya Shimoni. Kama sitanufaika na mradi huo mkubwa katika eneo langu la nyumbani, nani atanufaika? Ninajiandaa kwa siku zijazo. Utajiri huwajia walio wajasiri," anasema Bi Abdalla.

Akiwa amevalia buibui nyeusi, anatazama Bahari Hindi kwa makini na kueleza matumaini yake kwamba sekta ya uvuvi itasaidia kutatua shida ya ukosefu wa ajira nchini.

"Wazazi wangu walifurahia nilipowaambia nilichaguliwa kuwa mvuvi. Usaidizi wao umenipa nguvu. Mimi ndiye binti yao wa pekee na mdogo katika familia ya watoto wanne. Kakangu mkubwa ambaye pia ni mvuvi, ndiye alinihimiza nijiunge na sekta hii," anaongeza.

Teresia Kitindi, 23, kutoka Taita Taveta alikuwa akivutiwa na maji mengi. Hakuweza kupata kazi baada ya kumaliza Kidato cha Nne katika Shule ya Sekondari ya Voi, miaka minne iliyopita.

Mwaka wa 2020, aliamua kujaribu bahati yake katika mafunzo ya uvuvi yaliyofadhiliwa na serikali. "Hakuna kazi zilizotengewa wanaume au wanawake. Ninahimiza wanawake wa umri mdogo wajaribu bahati yao katika kila nafasi ya kazi wanayopata," anasema.



Mtafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Baharini na Uvuvi Kenya (KMFRI), Dkt James Mwaluma, akizungumza na wanahabari katika kiwanda cha samaki cha Liwatoni Septemba 6.
KEVIN ODIT I NATION

Maxine Ogenda, 23, alikuwa akisomea kozi ya Kuondoa na Kusambaza bidhaa katika Chuo cha Usimamizi wa Ushuru Kenya Mombasa alipopata habari kuwa serikali ilikuwa ikisajili wanawake kufunzwa uvuvi katika bahari kuu. Hakusita kutuma ombi lake.

"Uvuvi uko katika damu yangu. Wazazi wangu wako na mashua ndogo ambayo nimekuwa nikitumia kwa uvuvi. Nitakuwa mvuvi bora zaidi mwanamke," anasema.

Najma Machuyu, 25, yuko pia katika hali hiyo. Kifungua mimba huyo katika familia ya wasichana sita kutoka Kaunti ya Tana River, amekuwa akishiriki uvuvi kwa mashua ndogo tangu akiwa na umri wa miaka sita.

Amekuwa akitamani kuwa mvuvi lakini hakuwa na stakabadhi zinazohitajika kutafuta kazi. Alikuwa amefanya kozi ya kompyuta na alikuwa akifanya kazi katika duka la huduma za mtandao alipoona tangazo la kazi ya ndoto zake.

**Sh1 bn**

Serikali imetenga Sh1 bilioni kuwapa mafunzo vijana 1,000 kila mwaka.

Vivian Obondo anatoka Kaunti ya Homabay. Msichana huyu mwenye umri wa miaka 23 analenga siku za baadaye. "Hii ndiyo kazi nimekuwa nikitamani kufanya. Nataka kuelewa sekta ya baharini. Nataka kumiliki mashua zangu na kuajiri wanawake wenzangu," anasema.

Mwingine mwenye ari sawa ni Emily Doyo, 24, kutoka Tana River.

Kulingana na Mkurugenzi Msaidizi anayehusika na Uvuvi katika KMFRI, Nina Wambiji, serikali inataka kujenga uwezo wa vijana katika uvuvi, waelewe mfumo wa bahari ili waweze kushiriki katika uzalishaji kikamilifu. Anajivunia wasichana hao sita ambao wamepewa mafunzo.

"Wameamua kushiriki sekta ya baharini. Kwa kawaida, wanawake hawashiriki uvuvi wa chini ya bahari kwa sababu za kitamaduni na kidini na saa nyingi zinazotumiwa katika kazi hiyo. Kwamba wazazi wao wamewaruhusu kujiunga na sekta hii inayomilikiwa na wanaume ni hatua kubwa," anasema Wambiji.

Katika mashua ya 'The Jonas' pi kuna wanaume wanne vijana, na kufanya wanaopata mafunzo hayo kuwa kumi. Meneja Mkuu wa Pweza Fisheries, Jane Njeri,

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

anayemiliki mashua hiyo ya uvuvi, anasema aliamua kushirikiana na serikali kutambua na kujenga uwezo wa wanawake katika sekta hiyo.

Ndiye mwanamke wa kwanza kumiliki chombo cha uvuvi katika bahari kuu. Yeye na washirika wake wawili wanamiliki mashua zingine mbili. "Hizi ni mashua za kiwanda. Vijana hao kumi watafunzwa kuhusu uvuvi wa biashara.

Watakapoenda baharini, kila kitu kinafanyiwa kwenye mashua, ikiwemo kusafisha na kupakia, ili watakapofika ufuoni, samaki watakuwa tayari kupelekwa Ulaya na masoko mengine," anaeleza Njeri.

Lakini haitakuwa rahisi kwa wanabaharia hao wapya. "Tunatarajia mawimbi baharini na ninajua wataathiriwa na hali ya bahari, lakini tuko na dawa za kuwasaidia kwa hilo. Itakuwa tajiriba mpya kwao, kuwa mbali sana ndani ya bahari bila mtandao wa simu na bila dalili za maisha isipokuwa watu walio katika mashua na iwapo wana bahati, mashua nyingine inayopita."

Hajawahi kupeleka wanawake baharini awali, lakini anataka kuunda mazingira ambayo Kenya inaweza kuwa na manahodha wanawake na mabaharia, kama ilivyo katika sekta ya usafiri wa ndege. "Argentina ndiyo nchi ya pekee ninayojua iliyo na wahudumu wote wanawake wanaoenda kwenye bahari kuvua samaki. Kuna pesa katika uvuvi – karibu Dola 700 (karibu Sh85,000) kwa kiwango cha chini kwa kila tani ya samaki inayovuliwa," anasema Njeri.

**Kenya inatoa tani 160,000 za samaki kila mwaka ingawa ina uwezo wa kutoa tani 300,000. Takwimu kutoka KMFRI zinaonyesha kuna upungufu wa karibu tani 400,000 za samaki nchini.**

'The Jonas' itaenda hadi mpaka wa Kenya na Tanzania umbali wa karibu maili 240 baharini. Baada ya mafunzo, atawaajiri au awapendekeze kwa kampuni zingine.

Uvuvi katika bahari kuu Kenya, anasema, haujakumbatiwa kikamilifu. Mtaalamu huyo wa usimamizi wa shughuli za baharini aliishi Ulaya kwa miaka 15 kabla ya kurudi Kenya kuanza uvuvi. Huwa anauza samaki wake katika Muungano wa Ulaya, ambao ni soko gumu kuingia. Hasa anauza 'samaki wa upanga' (swordfish), ambao ni maarufu sana Italia, Uhisipania na Amerika na pia anauza aina nyingine wa samaki kama tuna na Kamba nane.

Serikali imewapa mafunzo vijana 408 kushiriki uvuvi katika bahari kuu tangu 2020 kufuatia agizo la Rais.

Wavuvi wa Kenya, anasema Afisa wa Huduma za Uvuvi, Mwaka Saidi, wamekuwa wakitegemea maji yaliyo karibu na fuo kwa kuwa hawana ujuzi na vifaa vya kutafuta samaki katika bahari kuu. Kenya inatoa tani 160,000 za samaki kila mwaka ingawa ina uwezo wa kutoa tani 300,000. Takwimu kutoka KMFRI zinaonyesha kuna upungufu wa karibu tani 400,000 za samaki nchini.

Kenya inalenga kuwapa mafunzo wavuvi 5,000 ili kutatua shida ya ukosefu wa ajira na kutuma wafanyakazi nje ya nchi. "Baada ya mafunzo, kuna nafasi za kazi zilizo tayari. Kwa wakati huu, vyombo vya uvuvi karibu na eneo letu vinahudumiwa na raia wa kigeni kutoka Afrika Magharibi, Ushelisheli na maeneo mengine. Tunataka waajiri watu wetu," anasema Mwaka.

Ingawa nchi inaruhusiwa kupatia leseni karibu vyombo 70 vya uvuvi katika eneo lake la bahari kuu, wavuvi wa Kenya hawana tekinolojia na vifaa vya kiviwanda vinavyohitajika kwa uvuvi katika bahari kuu.

Kwa kuwa sasa serikali imetenga Sh1 bilioni kuwapa mafunzo vijana 1,000 kila mwaka kuhusu uvuvi wa bahari kuu, nchi inaweza kunufaika kikamilifu kwa utajiri wake wa baharini.

**Wazazi wangu walifurahia nilipowaambia nilichaguliwa kuwa mvuvi. Usaidizi wao umenipa nguvu. Mimi ndiye binti yao wa pekee na mdogo katika familia ya watoto wanne. Ndugu yangu mkubwa, ambaye pia ni mvuvi, ndiye alinihimiza nijiunge na sekta hii.**

Fatma Abdalla




Naibu Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Baharini na Uvuvi Kenya (KMFRI), Dkt Nina Wambiji (wa pili kusho), akiwa na wanawake hao wachanga ambao wamegeuza majukumu ya jadi ya kijinsia kujitosa katika uvuvi wa maji makuu. PICHA I KEVIN ODIT

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

SUALA KUU

# VISIKI, MAGONGO HADI BUNGE

**MHESHIMIWA:** Bila pesa na bila familia yake mwenyewe, Peter Salasya alifaulu kushinda kiti cha Bunge cha Mumias Mashariki kupitia ucheshi wake, uaminifu na bidii ya kutimiza lengo lake.

● NA AMINA WAKO

Alidharauliwa kwa kukosa bibi na familia, lakini alipozunguka kuomba kura kwa kiti cha ubunge katika Uchaguzi Mkuu wa 2022, Peter Salasya alipuuza shutuma hizo, na kama kawaida kucheka tu huku akivuta mawazo ya wasikilizaji wake katika ajenda ya kampeni yake.

Salasya, 32, aliangua kicheko cha mwisho Agosti 9 alipochaguliwa Mbunge wa Mumias Mashariki na kuwa mmoja wa wabunge wachanga zaidi nchini.

Alizaliwa 1989 wa pili katika familia ya watoto saba. Salasya alilelewa eneo la Kisumu Ndogo, Kaunti ya Kakamega ambako alihudhuria Shule ya Msingi ya Shianderema na Shule ya Upili ya Lubinu Boys.

Baba yake aliaga dunia akiwa katika Kidato cha Pili na kuacha familia ikiwa hoi kifedha huku mama yake akibaki pekee yake kutafuta riziki.

"Ni kwa neema ya Mungu kwamba kumaliza shule. Nilifukuzwa mara nyingi kwa kukosa karo na wakati mwingine nilikaa nyumbani kwa siku nyingi mama yangu aakitafuta karo," anasema.

Alipoitwa kujiunga na Chuo Kikuu cha Egerton




Waziri wa Ulinzi, Eugene Wamalwa akifanya kampeni na Peter Salasya wa chama cha DAP-K katika soko la Shikanda, Kakamega, Agosti 5. PICHA I ISAAC WALE

## UONGOZI MPYA

With John Nyaga
jnyaga@ke.nationmedia.com

### MACHO YOTE KWAKE

GAVANA MPYA WA NAIROBI JOHN SAKAJA ALIANZA KAZI GHAFLA BAADA YA KUINGIA OFISINI AGOSTI 25. TAYARI AMENYAKUA KAZI YA KUKUSANYA USHURU KUTOKA KWA IDARA YAHUDUMA ZA JIJI LA NAIROBI MIONGONI MWA MAJUKUMU MENGINE, AKAAMURU KUACHILIWA KWA PIKIPIKI ZOTE ZILIZOKAMATWA NA KUONDOLEWA KWA KESI DHIDI YA WAENDESHAJI WAKE. AMEAPA PIA KUMALIZA DONDA SUGU LA UCHAFU JIJINI NAIROBI 'KATIKA SIKU CHACHE ZIJAZO', KULINGANA NA TAARIFA ZAKE KATIKA MITANDAO YA KIJAMII. KILA LA HERI MHESHIMIWA!!




### NYOTA WA WIKI

LINET CHEPKORIR, MAARUFU KAMA 'TOTO' AMEANDIKISHA HISTORIA KWA KUWA MWAKILISHI WA WANAWAKE MWENYE UMRI MDOGO ZAIDI BAADA YA CHAGUZI ZA AGOSTI 9.

BI CHEPKORIR, 24, ALIHITIMU CHUO KIKUU CHA CHUKA APRILI 2021. ALIWASHINDA WAGOMBEAJI WENGINE WANANE WALIOMZIDI UMRI KUWA MWAKILISHI WA TATU WA WANAWAKE KAUNTI YA BOMET.

WAPINZANI WAKE WALIPOTAMBA KAUNTI HIYO WAKITUMIA MAGARI MAZITO, BI CHEPKORIR ALITEMBEA HADI SEHEMU ZA KAMPENI NA WAKATI MWINGINE KUPEWA LIFTI ZA BODABODA NA WASAMARIA WEMA. SEMA KUJITOLEA!!



ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# 12,140

Kura ambazo Peter Salasya alipata kushinda kiti cha Bunge cha Mumias Mashariki . David Wamatsi wa ANC alipata kura 9,403, naye Benson Mapwoni wa UDA akapata kura 5,118.

kusomea Shahada ya Mauzo, kaka yake, James Salasia, aliahidi kugharamia masomo yake. Lakini miezi mitatu baada ya kujiunga na chuo kikuu, James aliachishwa kazi.

"Sikuwa na lingine ila kurudi nyumbani. Ilikuwa aibu kubwa kwangu baada ya kujipiga kifua kwa kufaulu kujiunga na chuo kikuu," anakiri.

Aliamua kumuomba Mbunge wake barua ya kupendekeza apewe ufadhili wa masomo kutoka Hazina ya Maendeleo katika Eneobunge (CDF). "Alisema hawezi kufanya hivyo. Badala yake alinishauri nifanye harambee akiahidi kutoa Sh5,000 kugharamia masomo yangu. Nilihisi vibaya sana na nikarudi nyumbani nikilia, kwa sababu nilifikiri huo ulikuwa mwisho wa elimu yangu," anasema Salasya.

Hatimaye, taasisi hiyo ilimruhusu kusoma bila kulipa chochote. Lakini kitendo cha Mbunge wake kilichochea ari ndani yake ya kugombea uongozi ili abadilishe maisha ya watu. Katika mwaka wake wa tatu chuoni, aligombea nafasi ya naibu mwenyekiti wa muungano wa wanafunzi na akashindwa.



Mbunge wa Mumias Mashariki, Peter Salasya, katika Majengo ya Bunge Septemba 8. PICHA | JEFF ANGOTE

Baada ya kukamilisha masomo na kufuzu 2013, Salasya alipata kazi kama muuzaji wa baiskeli, iliyomsaidia kuzunguka eneobunge zima la Mumais Mashariki. Alipokuwa akitangamana na watu mbalimbali, ndoto yake ya kuwawakilisha ilifufuka. Aliamua kuwania ubunge.

"Ilikuwa kama utani mkubwa. Utamaduni wa Waluhya unasema kiongozi ni sharti awe na nyumba, mke na familia yake. Sikuwa na chochote," anasimulia.

Mwishoni mwa 2017, Salasya alipata kazi ya benki. Kuwa kazini kwa saa nyingi hakukumpa muda wa kufanya kampeni na alishindwa vibaya katika chaguzi ambao aliibuka wa tatu kwa kura 254 pekee. "Ilikuwa uchungu. Niliona aibu na kuhisi kukataliwa na jamii yangu mwenyewe. Lakini niliamua kujizoa na kusonga mbele."

Alielekeza macho kwa uchaguzi mkuu wa 2022 na akaanza kujiandaa mapema kwa kuhudhuria hafla nyingi eneo hilo jinsi alivyoweza, zikiwemo za mazishi na harusi. Alianza pia juhudi za kufufua kiwanda cha sukari cha Mumias ambacho kilikuwa kitega uchumi kwa mamia ya wakulima wa miwa.

"Kutokana na masomo yangu kuhusu mauzo, nilielewa kilichokuwa kikitendeka kwa kampuni hiyo na nikawa nikiwafahamisha watu. Juhudi zangu za kufufua kampuni hiyo ziliniweka katika nafasi nzuri katika jamii," anafafanua Salasya.

Alifungua moyo pia kuhusu changamoto zake za kifedha. "Niliambia watu wazi kuwa sikuwa na pesa na bado wakakubaliana na mawazo na ajenda zangu. Ili kufidia hali yangu ya kukosa pesa za kampeni, nilibisha mlango wa karibu familia zote katika eneobunge na kuwaomba kura zao." Mambo yalianza kulainika taratibu. Kuhusu matangazo, alitumia mawe katika maeneo tofauti kubandika mabango yake ya kampeni.

Alishangaa wafuasi wake walipokusanya pesa kumjengea nyumba na kumwezesha

**Alizaliwa 1989 wa pili katika familia ya watoto saba. Salasya alilelewa eneo la Kisumu Ndogo, Kaunti ya Kakamega ambako alihudhuria Shule ya Msingi ya Shianderema na Shule ya Upili ya Lubinu Boys. Baba yake aliaga dunia akiwa katika Kidato cha Pili na kuacha familia ikiwa hoi kifedha huku mama yake akibaki pekee yake kutafuta riziki.**

> **Ni kwa neema ya Mungu kwamba kumaliza shule. Nilifukuzwa mara nyingi kwa kukosa karo na wakati mwingine nilikaa nyumbani kwa siku nyingi mama yangu aakitafuta karo.**
>
> Peter Salasya

kutimiza angalau moja la matarajio ya jamii kwa kiongozi.

Bado hakuwa na mke, ingawa haimaanishi hakuwa amejaribu. Mpenzi aliyekuwa akiishi naye alimtema na kumwendea mwanamume tajiri kumshinda kabla ya chaguzi kwa sababu "singeweza kumudu mtindo wake wa maisha."

Salasya alijiunga na chama cha DAP-Kenya baada ya kukosa tiketi ya ODM. Jinsi ilivyotokea, hii ilikuwa hatua mwafaka. Alishinda kiti hicho kwa kura 12,140 na kuwa Mbunge wa pekee kuchaguliwa kwa tiketi ya DAP-Kenya. Aliwashinda wapinzani wake David Wamatsi wa ANC (kura 9,403) na Benson Mapwoni wa UDA,(kura 5,118).

Ajenda yake ni kuhakikisha usawa katika ugavi wa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wasiojiweza katika eneobunge hilo, kuinua viwango vya elimu, kuimarisha vijana na wanawake na kufufua Kiwanda cha Sukari cha Mumias.

Anawashauri vijana wanaopanga kujitosa kwenye siasa: "Weka Mungu mbele, kuwa na ndoto na ujikubali. Usijibadilishe ili utoshee, zungumza na watu unaotaka kuwakilisha na utangamane nao mara kwa mara."

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

taharıri




■ Hatua ya dharura inahitajika: Hasira na ama kisasi zitafunika akili na maono yake

# Bw Rais, ni wakati wa kuunganisha taifa



KWENDO **OPANGA**

NAIBU Rais William Ruto, ambaye alisutwa kwa kuitwa mwizi mkubwa, mporaji wa pesa za umma na aliyeeneza uongo wakati wa kampeni zake, Jumanne ataapishwa kuwa rais. Ruto, ambaye alikataliwa na Rais Uhuru Kenyatta na ambaye rais alimpinga wazi na kumpuuza kuwa mtu asiyefaa kuongoza, alitangazwa mshindi wa uchaguzi wa urais wa Agosti 9 na kudumishwa na Mahakama ya Upeo Jumatatu.

Rais, ambaye hajampongeza Ruto, hata hakumtaja kwa jina alipotoa taarifa kuhusu uamuzi wa mahakamakortie.

Kwa hasira, Rais Kenyatta alishangaa ni kwa nini mahakama ilitoa uamuzi kwa njia fulani katika uchaguzi mmoja na njia tofauti katika uchaguzi mwingine. Naibu Rais ambaye alidharauliwa na maafisa wa vyeo vya chini katika chama tawala, na kurushiwa matusi hadharani na mawaziri wa serikali, atashikilia afisi kubwa zaidi nchini.

Kwa hivyo, Dkt Ruto atakapokuwa akiapishwa kuwa Rais, sharti akumbuke kuwa hasira na ulipaji kisasi hazijengi kiongozi.

Sharti apate funzo kwamba kampeni zilizojaa hasira ambazo yeye na wapinzani wake waliendesha, hazina manufaa yoyote. Dkt Ruto anafaa kusahau hayo na kuelekeza juhudi zake katika kazi ya kustawisha nchi hii. Ni marehemu Mario Cuomo, mwanachama wa chama cha Democrat, na aliyekuwa gavana mara tatu wa jiji la New York, aliyesema kuwa unafanya kampeni kwa ushairi lakini unaongoza kwa riwaya. Hotuba na matamshi yaliyotolewa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa Agosti 9, hayakuvutia. Yalijaa matusi na kauli za kushusha hadhi. Lakini kama Rais, sharti Ruto akumbatie uongozi unaoheshimu utu, ungwana na adabu. Rais Ruto ni lazima abebe Bibilia yake, hasa Agano Jipya (tuwasamehe waliotukosea) na sio Agano la Kale ( jicho kwa jicho).

**Ruto atatambua kuna wengi miongoni mwa matabaka ya wanasiasa na matajiri ambao watampuuza. Wanasikia kauli mbiu yake ya hasla kuhusu mtoto wa masikini ambaye alipanda ngazi hadi kilele cha uongozi. Lakini wanashuku tabaka lake na chanzo cha utajiri wake.**

Katika mfano mzuri wa kuelekeweka vibaya kwa hadithi ya Kiarabu, Ruto alibandikwa jina Ali Baba huku mpinzani wake, Raila Odinga akitajwa kuwa Baba. Ali Baba alichukuliwa kuwa mwizi na kiongozi wa genge la wezi 40 ambao walikuwa tayari kuibia Kenya.

Ali Baba hakuwa mwizi, hakuongoza genge lolote la wezi. Alikuwa mpasua mbao asiye na doa, aliyeingia kwa bahati kwenye pango ambako wezi 40 walikuwa wameficha mali.

Alisikiliza mazungumzo yao na kufahamu nambari ya siri ya mlango wa kiajabu. Hapo ukafunguka! Sharti Rais Ruto awaaibishe waliomwekelea kosa la kupora mali ya umma, kwa kulinda rasilimali za umma, kuhakikisha afisi za umma zinawajibika na kuhakikisha maafisa wa usalama na idara ya mahakama zinahudumia Wakenya kwa usawa. Kwa hivyo, ingawa Ruto alisema asasi za usalama hazitatumiwa kuandama wapinzani wa kisiasa, sharti ahakikishe hazitatumiwa kufunika maovu yanayotendewa watu.

Ruto atatambua kuna wengi miongoni mwa matabaka ya wanasiasa na matajiri ambao watampuuza. Wanasikia kauli mbiu yake ya hasla kuhusu mtoto wa masikini ambaye alipanda ngazi hadi kilele cha uongozi. Lakini wanashuku tabaka lake na chanzo cha utajiri wake.

Mahasla wanamtaka Ruto awafanye matajiri. Matajiri nao wanamtaka alinde mali yao. Wengine wanaamini ni wakati wao kula. Wengi, hata hivyo, wanataka serikali iwafanyie kazi na Ruto atimize ahadi ambazo alitoa ili waimarishe maisha yao.

Hakuna hata moja kati ya haya ambalo ni shairi. Yote ni riwaya, hasa Ruto atakapoingia ofisini mwaka na kupata barua inayosema: Hatua ya Dharura Inahitajika: uchumi umeharibiwa na Covid – 19, umenyongwa na madeni na kutishwa na kudorora kwa uchumi ulimwenguni.

Hasira na ama kisasi zitafunika akili na maono yake. Lakini kwanza sharti alete pamoja na kuunganisha Wakenya ambao yeye na wapinzani wake waligawanya.

*kwendo58@gmail.com*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni

Shabaha kuu ya mpiganiaji uhuru si kuwa rais tu, bali kukomboa watu kisiasa na kiuchumi

# Japo Raila alishindwa, jina lake liko katika orodha ya watu mashuhuri Afrika



MACHARIA GAITHO

Raila Odinga anapitia mambo kadhaa baada ya kushindwa; kuvunjika moyo, hasira na kinyongo kwa kuhisi kuwa watu walimsaliti. Lakini ana namna ya kubadili hali hiyo.

Inavunja moyo kwa mtu yeyote yule kushindwa mara tano katika uchaguzi wowote ule, hasa baada ya kufanya kazi nzuri ambayo imetambuliwa na wananchi na kumletea sifa tele.

Kwa sababu hiyo, inatia moyo kuona kuwa amekubali hali hiyo. Ingekuwa vibaya kama angemalizia safari yake ya kisiasa kwa kugeukia vitendo vinavyoweza kumuingiza pabaya.

Kwa umri wake wa miaka 77, itabidi akubali kuwa hawezi tena kugombea urais. Tayari ameonyesha kuwa kushindwa mara tano katika uchaguzi wa urais, pamoja na kupokonywa ushindi mara mbili kwa ulaghai, si mwisho wa dunia.

Raila bado ana mengi ya kufanya, hasa baada ya kubaini kwamba kuwa rais si jambo pekee analofaa kulenga kutimiza maishani mwake.

Ingawa hajawahi kuwa rais, amechangia zaidi ustawi wa kisiasa na kijamii nchini kuliko mtu mwingine yeyote yule, tangu mashujaa walioongoza vita vya uhuru.

Anaweza kukumbuka mashujaa wengi wa kupigania uhuru na haki za biadamu kote duniani, ambao hawakuwa marais, lakini mafanikio yaikuwa makubwa kuliko ya wenzao walioyatumia kama ngazi kuwa marais wa nchi husika.

Mpiganiaji uhuru hatambuliwi kwa kuwa rais tu bali kwa kuongoza watu kujinasua kutoka kwa minyororo ya kisiasa, kiuchumi na kimawazo.

Kama si kujitolea kwa watu kama Dedan Kimathi, Jomo Kenyatta, Oginga Odinga, Harry Thuku, Achieng' Oneko na wengine waliokuwa mstari wa mbele kuwakabili wakoloni,

Tamaaya kupata uhuru haingetokea katika mawazo ya watu kama mashujaa hao hawangeonyesha njia. Pengine Kenya ingeendelea kuwa chini ya utawala wa kikoloni kwa miaka mingi zaidi.

Vivyo hivyo, ni Raila – akishirikiana na mashujaa wenzake Kenneth Matiba, Charles Rubia, Masinde Muliro, Paul Muite, Henry Okullu, Gitobu Imanyara, Timothy Njoya na Oginga Odinga ambao walipagana dhidi ya mfumo wa kidikteta wa utawala wa chama kimoja. Uhuru tunaofurahia leo ni kazi ya walioongoza vita vya Ukombozi wa Pili.

Si mashujaa wote walioishi kuona na kufurahia matunda ya juhudi zao. Wengi walikufa wakipigana, au baada ya ushindi walitemwa na wengine ambao hawakupigana au hata walioshirikiana na wadhalimu.

Hiyo ndiyo hali ya maisha, ambayo pia inatukumbusha kuwa wanaopigania uhuru hawafanyi hivyo kuchukua nafasi ya wadhalimu katika mamlaka, bali kuhakikisha watu wao wako huru.

Jina la Raila liko katika orodha ya watu wanaoheshimika Kenya na Afrika nzima. Kama mkombozi, mpiganiaji mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, mtu mwenye maono, anamzidi kwa mbali Rais-mteule William Ruto, rais anayeondoka Uhuru Kenyatta na watangulizi wao wawili, Mwai Kibaki na Daniel arap Moi. Hata asipogombea urais tena, Raila ana kazi nyingi ya kufanya ya kuongoza vikosi vya kupigania uongozi bora Kenya.

Awamu inayofuata ya maisha yake si ya kupinga serikali ya Ruto, bali kuendelea kupigania ukombozi wa kijamii na kiuchumi.

**Kama mkombozi, mpiganiaji mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, mtu mwenye maono, anamzidi kwa mbali Rais-mteule William Ruto, rais anayeondoka Uhuru Kenyatta na watangulizi wao wawili, Mwai Kibaki na Daniel arap Moi.**

Tayari, tumeona viongozi wenye tamaa wanavyosaliti wapigakura wao kwa kuhama Azimio na kujiunga na Kenya Kwanza, kwa manufaa yao binafsi. Muungano wa Azimio unahitaji uongozi thabiti wa kudumisha nidhamu, uwajibikaji na kujitolea ili wanasiasa wake katika Bunge la Kenya na serikaliza kaunti waweze kutimiza wajibu wao kuhakikisha serikali inafanya kazi ipasavyo.

Serikali yoyote isiyolazimishwa kuwajibika inaweza kuturudisha enzi za giza za ukiukaji wa haki za binadamu na wizi wa mali ya umma.

Raila hawezi kustaafu kwa sasa; ana wajibu wa kulea kizazi cha viongozi ambacho hatimaye kichukua nafasi yake.

*gaithomail@gmail.com*

# Kutoka hekima ya Suleimani hadi 'ínky pinky ponky', tamati ni mwisho



ALLAN BULUKU

Nusura nchi ichanganyikiwe wiki iliyopita mawakili wakuu wakipigana mieleka ya kitaaluma katika Mahakama ya Upeo kuhusu matokeo ya kura ya urais. Mawakili wakuu walishangaza kina yahe kwa umilisi wao wa sheria. Majaji wanastahili sifa; walikuwa watulivu wakati wote wa makabiliano hayo, huku nyimbo za chekechea zikiibuka kortini.

Mambo mengi yamesemwa kuhusu "wanaume na wanawake hao saba wenye hekima" tangu uamuzi walliotoa Jumatatu. Lakini shtaka moja ambalo hawawezi kuwekelewa ni kuwa hawana nguvu. Wakiwa wamevalia magwanda yao rangi nyekundu na nyeusi, Majaji wa Korti ya Upeo hawakuvunja moyo. Kutoka kwa nukuu za Bibilia za Jaji Smokin Wanjala hadi hekima ya Suleimani ya Jaji Philomena Mwilu, saba hao waliangaza nchi kwa mng'ao wa ajabu.

Baadhi ya mawakili walijiabisha wenyewe kwa majibu yasiyoridhisha huku wengine wakiwasilisha "ushahidi" ambao ulibadilika kuwa "hewa na usiotimiza lengo lolote", walivyosema majaji - tamko ambalo lilizua hasira miongoni mwa baadhi ya wachanganuzi.

Hatimaye, uamuzi lazima ungetolewa. Waliounga mkono walalamishi waliteta kuhusu lugha aliyotumia Jaji Mkuu Martha Koome katika mukhutasari wa uamuzi aliosoma. Lakini jaji huyo anayependwa, mwanamke mwenye moyo safi ambaye hawezi kuumiza yeyote, alisema ilikuwa "kazi ya Mungu".

Huku ukitamatisha vita vikali vya kuelekea Ikulu kati ya Rais-mteule William Ruto na mgombea urais wa Azimio la Umoja - One Kenya Raila Odinga, uamuzi huo uliacha sehemu moja ya nchi ikiwa imevunjika moyo.

Hakika, maneno ya Jaji Mwilu yalielezea ukweli wa mambo aliposema: "Zaidi ya wapigakura milioni sita watalipuka kwa furaha tele huku wengine idadi sawa na hiyo wakitamauka kabisa. Hata hivyo, hivyo ndivyo ilivyo kazi tunayofanya."

Mwaka wa 2000, jambo sawa na hilo lililitendeka Amerika. Katika mmoja wa chaguzi zilizozua ubishi mkali katika historia ya Amerika, Mahakama ya Upeo iliamua George W Bush wa chama cha Republican alikuwa mshindi baada ya kukabana koo na Al Gore katika kura za jimbo la Florida. Bush alidai alikuwa ameshinda kwa kura 537.

Hapa kwetu, Rais-mteule Ruto aliepuka raundi ya pili ya uchaguzi wa kura kwa kura 69,000. Naam, pole pole Kenya inaendelea kupata imani kwa hesabu ya kura. Mahakama ya Upeo imefanya kazi yake, na wengine, kama gazeti la 'The New York Times', ambao walikuwa na maoni kwamba nchini Kenya watu hupiga kura na kusubiri Mahakama ya Upeo 'kuteua' Rais, wanafaa kupuuzwa kabisa na Wakenya.

Hali inaendelea kutulia na wiki hii, tutaapisha Rais mpya kwa mujibu wa Katiba ya 2010. Ni mwanzo mpya kwa nchi. Ni sharti tufanye hivyo kwa kujivunia ufanisi wetu.

*abuluku@ke.nationmedia.com*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

KUPAA NA KUSHUKA KWA FAMILIA YA MOI

# GIDEON AACHILIA RUNGU

*Ndoto za himaya ya kisiasa katika Bonde la Ufa zinaonekana kuwa mhasiriwa wa kwanza wa kuinuka kwa Ruto kuwa rais wa Kenya.*

• Na JOHN KAMAU



Kudidimia kwa chama cha jogoo: Aliponoa katika siasa, Gideon Moi alifidia zaidi katika biashara na mchezo wa polo.

Kinyume na baba yake, aliyekua akichunga mbuzi, Gideon Moi alilelewa akicheza mchezo wa 'Polo'. Akiwa na baba bilionea tajiri, Rais Daniel arap Moi, na rafiki mashuhuri wa familia yake, Mwanasheria Mkuu Charles Njonjo, Gideon alikuwa kizazi cha kipekee – lakini si kwenye ulingo wa siasa.

Kaka yake mkubwa, Jonathan, akipendelea mashindano ya mbio za magari, Gideon alikuwa mfugaji wa farasi wanaoshiriki mchezo wa 'Polo', uraibu aliogeuza kuwa biashara.

Katika maisha yake ya kifahari, hata hivyo, Gideon amekuwa na farasi wengi kuliko marafiki wa kisiasa. Ni Katibu Mkuu wa Kanu, Nick Salat, pekee anayeweza kuhesabiwa kama mwandani wake wa karibu kisiasa.

Lakini mstakabali wa Nick ulizikwa pamoja na himaya ya Moi tufani kali ya Rais-mteule William Ruto iliposomba Bonde la Ufa katika Uchaguzi Mkuu uliokamilika majuzi.

Kwa miaka 67 iliyopita – tangu 1955 – familia ya Moi imekuwa na angalau jamaa wake mmoja katika bunge la nchi, chini ya utawala wa kikoloni na baada ya uhuru.

Katika miongo miwili iliyopita, wanawe wawili Mzee Moi, Gideon na Raymond, wamekuwa wabunge – japo hakuna kati yao aliyeweza kupata uungwaji mkono wa kitaifa katika eneo hilo ilivyokuwa kwa baba yao.

Kabla ya kujiunga na siasa, Gideon alikuwa tu anafahamika katika nyanja za 'Polo' na biashara mbalimbali. Wananchikenya walifahamu machache kumhusu. Jina lake lilianza kutajwa siku chache kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 1997, alipokusanya marafiki zake kutoka bara Asia kuchangisha pesa za kampeni za Kanu.

Tofauti na kampeni za awali, mnamo 1992, pesa zilizoporwa kwenye kashfa ya Goldenberg zilifadhili kampeni. Chama tawala kiligeukia mabwenyenye waliokuwa wamejitajirisha kutokana na "makuu" yaliyoambatana na kupigia debe serikali.

Gideon, ambaye alisomea Chuo Kikuu cha Salford, alikuwa na uhusiano wa karibu zaidi na ndugu zake. Mwandishi wa wasifu wa Moi, Andrew Morton, alitaja hili pia. "Moi hakuwa na furaha katika familia yake isipokuwa pengine kutoka kwa Gideon na June, Rais anahisi kukatizwa tamaa na kuvunjwa moyo na watoto wake. Ni wazi kuwa, kinyume na enzi za Kenyatta akiwa rais, ni nadra kwa familia yake kuhudhuria hafla za kitaifa kama vile Sikukuu ya Madaraka, kumhimiza."

Aliyekuwa akipigiwa debe awali kumrithi Rais wa zamani kwa kiti cha ubunge Baringo ya Kati ni mwenyekiti wa Benki ya Cooperative wakati huo, Hoseah Kiplagat, kigogo mashuhuri katika enzi za Moi.

Lakini katika mkutano wa Novemba 2002 uliofanywa katika shamba kubwa la makonge la Gideon, Alphega Sisal Farm, mjini, Koibatek, na kuhudhuriwa na Kiplagat, Gideon alipendekezwa na wajumbe 3,000 wa Kanu kurithi kiti cha baba yake.

Wakati huo aliweza kutamka maneno machache tu ya Kiswahili, ambayo kwa hakika hayakutosha kuhutubia mkutano wa kisiasa.


Kulingana na ripoti za vyombo vya habari, hotuba yake ya kukubali uteuzi huo haikuwa rahisi na ilijaa lafudhi nzito ya Kiingereza. Kujitokeza kwa Gideon mnamo 2002 katika kinyang'anyiro cha ubunge Baringo ya Kati kulitatiza hali – hasa kwa waliokuwa wanapinga kuinuka kwa utawala wa Moi.

Wapinzani wake watano walitoa taarifa ya pamoja Nakuru, wakiahidi kupambana na Gideon na kumshutumu Moi kwa "kuandaa mwanawe kumrithi. Ni kinyume na demokrasia," wakasema. Watano hao walikuwa Katibu Mkuu wa chama cha Safina, Juma Kiplenge; mkosoaji wa Moi na mgombea wa Social Democratic Party (SDP), Amos Kandie, aliyekuwa amegombea dhidi ya Moi 1997 na kupata kura 210 pekee huku Moi akipata kura 38,015; wakili Thomas Letangule, aliyegombea kwa tiketi ya National Rainbow Coalition, na limbukeni wawili wa kisiasa Raymond Kenei na Isaiah Cherutich.

Hadi leo haijawahi kujulikana kilichotendeka kati ya hotuba hiyo kwa wanahabari na Uchaguzi Mkuu wa Disemba 27, 2002, – kinachofahamika ni kuwa wote walijiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho na kumuacha Gideon kuwa mgombeaji wa pekee akaingia Bunge bila kupingwa.

Gideon Moi alitamausha bungeni; ilikuwa nadra kwake kuzungumza. Alianza kwa kishindo, kushambulia urais wa Kibaki lakini akakimya alipotajwa kwenye kashfa ya Goldenberg.

Mnamo 2020, alikuwa miongoni mwa maseneta waliotajwa kama "wabunge wasiozungumza" na shirika la kuangazia bunge kutokana na mchango wao finyu bungeni.



Kinara wa Kanu Gideon Moi akiwa na Rais -mteule William Ruto.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

Mwaka uliopita, Gideon, kwa mara nyingine alikuwa miongoni mwa wenye utendakazi mbaya zaidi, kulingana na ripoti iliyotolewa na Hazina ya Mzalendo, ikizingatia mara alizozungumza bungeni kulingana na rekodi za Hansard.

Gideon alifidia udhaifu wake wa kisiasa katika biashara na mashindano ya Polo. Baada ya kutumia siku yake kwenye shughuli za biashara, angeungana na mwandani wake wa miaka mingi na mmiliki wa ardhi Laikipia, Cindy Voorspuy, Anthony Kegode, mchungaji wa Kimaasai, aliyegeuka kigogo wa kimataifa wa mchezo wa Polo, marehemu Simon Kuseyo, na mfanyabiashara Phillip Arunga kucheza 'Polo'.

Wakati mmoja 1997, Gideon alikuwa mwanachama wa timu ya wachezaji Waafrika inayofahamika kama Black Rhinos, iliyoshinda Kombe la kwanza la Kitengela Birthday Cup lililoanzishwa na mmiliki wa hoteli na mpishi Rolf Schmid, ambaye hoteli yake ya Red Bull ilikuwa maarufu kwa matajiri wa eneo hilo.

Ingawa ujenzi wa himaya ya kisiasa ya Moi ulionekana kuwezekana kupitia Gideon na Raymond kuingia katika siasa za kitaifa, uvamizi wa Raila Odinga kwa chama chake cha Orange Democratic Party (ODM) mnamo 2007 ulizamisha ngome ya Kanu ya Bonde la Ufa.

Ruto, kupitia chama chake cha United Democratic Alliance (UDA), alididimiza kabisa Kanu katika Bonde la Ufa ambako ni Julius Sunkuli na William Kamket walionusurika makombora ya UDA katika maeneo ya Kilgoris na Tiaty mtawalia.

Gideon alikuwa na ndoto ya urais, ingawa alikosa taswira na ukakamavu wa mwanasiasa. Alipozungumza, alikuwa mpole na maneno yake yalitamkwa kwa makini.Wenyeji walimchukulia kuwa mtu asiyependa kutangamana na watu, labda alijitenga sana na matatizo yao.

Moi alipougua, Gideon alijitokeza kama msemaji wa familia – na kuamua ni nani angemtembelea mzee Moi nyumbani kwake Kabarak, na ni nani angezuiwa kumuona.

Ruto, aliyekuwa hasimu wake, alidaiwa kunyimwa nafasi ya kumuona Moi. Lee Njiru, msemaji wa aliyekuwa rais, alisema ziara ya Dkt Ruto "ilitokea wakati ule ule Mzee Moi alikuwa akifanya mazoezi yake ya kawaida na madaktari wake."

Kufuatia kifo cha baba yake mnamo Februari 2020, Gideon alipewa "rungu ya nidhamu" – inayoashiria uongozi wa kisiasa – iliyoonekana kuonyesha utawala wa Moi ulikuwa unaelekea kuundwa upya na ngome ya Bonde la Ufa.

Ndoto hiyo haipo tena, ikizingati-

■ MBOYA ALIKUWA WA KWANZA, SASA HAZIPO TENA

# 'Kifo' cha Jezi maarufu za kampeni

• Na JOHN KAMAU

HAPO awali, jezi zenye picha za wagombea nafasi tofauti za kisiasa ndizo zilikuwa zikitumika kama njia kuu ya kuwafikia wafuasi wao.

Hata hivyo, hali imebadilika. Kuna njia nyingine za kisasa ambazo zimeibuka kuwa maarufu na zenye mvuto zaidi.

Kwenye uchaguzi mkuu wa juzi, bei ya wastani ya jezi moja ilikuwa Sh200. Wagombea wengi hata hivyo waliamua kutumia mabango au mitandao kuendeleza kampeni zao. Hivyo, matumizi ya jezi kama njia ya kampeni yanaendelea kupungua.

Tangu majeshi ya Amerika yalipovumisha matumizi yake wakati wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, jezi ziliibuka kuwa vazi maarufu sana, hasa miongoni kwa watu walioajiriwa.

Hata hivyo, zilitumika mara ya kwanza na Thomas Dewey mnamo 1948 kwenye kampeni zake kuwania urais nchini Amerika. Alizitumia kama njia ya kuwasiliana na wafuasi wake ili kupata umaarufu zaidi.

Ijapokuwa mwanasiasa huyo alishindwa kwenye uchaguzi huo na Harry Truman, uvaaji jezi uliibuka kuwa maarufu kama vazi la kawaida, watu wasipokuwa kazini.

Hapa Kenya, Tom Mboya ndiye alikuwa mwanasiasa wa kwanza kuvaa jezi hadharani, alipofika mahakamani mnamo 1958 kwenye kesi ya uhalifu dhidi ya wabunge wote saba Waafrika wakati huo.

Mboya alifika mahakamani akiwa amevaa jezi kutoka Amerika na vazi jingine kutoka Ghana. Kutokana na upekee mkubwa wa kimavazi, aliangaziwa sana na vyombo vya habari.

Kwenye uchaguzi wa 1961, Mboya alitengeneza jezi zenye picha ya Mzee Jomo Kenyatta, wakati huo akiwa bado gerezani. Hiyo ndiyo ilikuwa mara ya kwanza kwa jezi kutumika kwenye kampeni nchini.

Mboya alikuwa akiendeleza harakati za kushinikiza serikali ya kikoloni kumwachilia Mzee Kenyatta kutoka kifungo cha nyumbani.

Katika miaka ya 1960, watu wagombea ubunge walikuwa wakichapisha picha zao kwenye jezi ili kutofautisha wafuasi wao katika kampeni za pamoja za Kanu. Kwenye kampeni za uchaguzi wa 1974, vyombo vya habari viliripoti kuwa wanasiasa walitumia hadi Sh15 kutengeneza jezi moja yenye picha.

Wakati huo, picha zilizotumika ni rangi nyeusi na nyeupe tu, kwani tekinolojia na kiwango cha utengenezaji bado kilikuwa chini.

Licha ya mtindo wa kuendesha kampeni za pamoja kukamilika mnamo 1979, wagombea tofauti walitengeneza jezi ili kuendeleza vyama vyao. Hali hiyo iliendelea kupata umaarufu zaidi baada ya marehemu Daniel Moi kujitosa siasani kwa kishindo, akitumia kauli mbiu "Nyayo." Hilo lilimfanya kutengeneza maelfu ya jezi zenye maandishi "Fuata Nyayo."

Matumizi ya jezi yalifikia upeo baada ya Kenya kuanzisha mfumo wa vyama vingi vya kisiasa mwanzoni mwa miaka ya tisini.

Hilo pia lilichangiwa sana na ujio wa vuguvugu la Youth for Kanu'92 (YK'92), lililoanzishwa kumfanyia kampeni Moi. Vyama vikuu vya upinzani - Ford Kenya na Ford Asili - pia vilikumbatia mtindo huo.

Mrengo wa mwanasiasa Kenneth Matiba katika chama cha FORD (kabla ya kuvunjika) uliwashtua watu wengi baada ya kusafirisha maelfu ya vijana wakiwa wamevalia jezi zenye picha ya Bw Matiba.

Vile vile, chama cha DP, chake Mwai Kibaki, kilitengeneza maelfu ya jezi za vijana.

Kwenye kampeni za muhula wa kwanza wa serikali ya Jubilee, maelfu ya jezi zilisafirishwa nchini kwa makontena kadhaa, baada ya kutengenezewa nchini China.

Kutokana na ongezeko la wahudumu wa bodaboda nchini, wanasiasa sasa wamewageukia kama njia ya kuendesha kampeni zao.

Hata hivyo, hali imebadilika nyakati hizi, kwani wagombea wengi wanatumia mitandao ya kijamii na njia nyingine za kidijitali kuwafikia wafuasi wao.



Katika miaka ya 1960 wagombea ubunge walichapisha picha zao kwenye jezi ili kutofautisha wafuasi wao katika kampeni za pamoja za Kanu.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## Sayansi na Teknolojia

# Hatimaye Twitter yakubali ombi la watumiaji la kitufe cha kuhariri

Na AFP

Twitter, hatimaye inawapa watumiaji wake kifaa kipya ambacho wamekuwa wakiomba sana - kitufe cha kuhariri jumbe.

"Ukiona ujumbe uliohaririwa, ni kwa sababu tunafanyia majaribio kitufe cha kuhariri. Hili linafanyika na utakuwa sawa," kampuni ikasema kwa ujumbe wa Twitter.

Kampuni inaendelea kufanyia majaribio huduma hiyo mpya na itaizindua katika wiki zijazo kwa watumiaji wa Twitter Blue, kwa gharama ya dola $4.99 (karibu Sh600) kwa mwezi.

Jumbe za Twitter zitaweza kuhaririwa mara chache katika muda wa dakika 30 baada ya kutumwa. Twitter kwa sasa inapatikana Amerika, Canada, Australia na New Zealand - lakini majaribio ya kwanza yatakuwa katika nchi moja tu.

Jumbe za Twitter zilizohaririwa zitatokea zikiwa na alama, muhuri wa wakati zilipohaririwa na kiuzi cha kuonyesha "Historia ya Uhariri" ili kulinda uadilifu wa mawasiliano na kuweka rekodi inayoweza kupatikana na mtu yeyote kuhusu yaliyosemwa," ikasema kampuni ya Twitter katika mtandao. "Mawasiliano kwa Twitter yatakuwa rahisi na ya kuvutia," ikasema Twitter.

"Utaweza kushiriki mazungumzo kwa njia ya kuvutia na tutaendelea kuimarisha njia za kuonfoa ugumu wowote wa kufanya hivyo."

Mwanzilishi mwenza wa kampuni hiyo, ambaye alikuwa Afisa Mkuu Mtendaji, alikuwa amesema huenda haingetoa kifaa hicho. Lakini mnamo Aprili, Elon Musk, akipanga kununua kampuni hiyo wakati huo, aliweka kura ya maoni katika Twitter na 73.6 ya watu 4.4 milioni walioshiriki wakasema walikitaka. Lakini kuna baadhi wanaosema si cha lazima na ama ni kinyume cha lengo la mtandao wa Twitter.

# JIJI KUU KATIKA JANGWA



Na HILARY KIMUYU

Hakuna barabara, magari ama moshi, ni mita mia 200 tu upana, lakini kilomita 170 urefu na mita 500 juu ya bahari, karibu 'The Line', jiji lonalopigiwa debe kuwa la jengo moja jangwani, ambalo hatimaye litakuwa makao ya watu milioni tisa.

Mwezi uliopita, Saudi Arabia ilizindua mchoro wa mradi wa jiji la kisasa, linaolenga kubadilisha eneo la kaskazini magharibi mwa falme hiyo.

Jiji hilo linatarajiwa kuwa na upana wa mita 200, urefu wa kilomita 170 na mita 500 juu ya bahari. Jiji hilo, kwa jina 'The Line', linatarajiwa kuwapa makao watu milioni tisa.

Kulingana na mchoro, jiji hilo litazungukwa na ua pande zote. Linatoka katika Bahari ya Shamu kuelekea eneo la mashariki kwenye jangwa na milima.

Jiji hilo la kipekee ni sehemu ya mradi wa serikali wa Neom,

unaolenga kustawisha eneo hilo. Serikali ilitoa video maalumu zikionyesha kuta ndefu za mji huo mbazo zimezunguka miti, bustani na maeneo ya burudani.

Taswira ya kwanza ya mradi huo ilionyesha majengo mawili

sambamba, yenye vioo vitakavyokuwa vikitumika kama kuta za nje. Mwanamfalme Mohammed bin Salman, alisema jiji la 'The Line' litakuwa na vioo ambavyo vitaonyesha taswira ya jangwa linalouzunguka.



**Michoro katika stakabadhi za ujenzi wa jiji la 'The Line' ikionyesha jengo linaloanzia Ghuba ya na kupasua mlima sambamba na pwani. Jiji hilo linaloendela kujengwa nchini Saudi Arabia, eneo la Neom, Tabuk, linasemekana halitakuwa na magari, barabara wala vifaa vyovyote vinavyotoa moshi.**

Taasisi nyingi katika jiji hilo, zikiwemo shule, makao ya watu na afisi zitapangwa kwa muundo wa jumba la orofa.

Ingawa maelezo kamili kuhusu jiji hilo bado ni haba, waliouchora wwanadai litategemea kawi asilia kuendesha shughuli zake, bila barabara, magari wala moshi. Reli ya kisasa itaunganisha sehemu za 'The Line', inasema taarifa kwa vyomba vya habari kutoka kwa Neom.

Mradi wa Neom, ambao ulitangazwa 2017 ni mpango wa Mwanamfalme Mohammed wa kugeuza eneo la jangwa lisiloishi watu kuwa jiji la kisasa linalojitegemea kwa mambo mengi.

Ni sehemu ya mipango ya kuvutia wawekezaji wa kigeni na kupanua uchumi wa Saudi Arabia mbali na kutegemea tu uuzaji wa mafuta.


Ujenzi tayari umeanza huku watu 1.5 milioni wakitarajiwa kuwa wakazi wa mji wa 'The Line' ifikapo 2030. Mwaka uliopita, mwanamfalme alisema ujenzi huo unaweza kugharimu hadi dola 200 bilioni (karibu ShSh24 trilioni), lakini wakati huo mchoro wake haukuwa umebadilishwa kujumuisha majumba mengine makubwa ya chini.

Wachoraji wa jiji hilo wanasema hali yake ya hewa itakuwa bora mwaka mzima kutokana na mseto wa vivuli, miale ya jua na sehemu nyingi na kubwa za kuingiza hewa safi.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya Afrika

■ VITA VYA UKRAINE VYATIKISA UHUSIANO WA URUSI NA AFRIKA




Rais wa Urusi Vladimir Putin (katikati) apigwa picha na viongozi wa nchi za Afrika waliohudhuria kongamano la kiuchumi kati ya Urusi na Afrika jijini Sochi, Urusi, Oktoba 24, 2019. PICHA | AFP

# URUSI YAPOSA AFRIKA TENA

*Tangu 2019, Urusi imekuwa ikifanya juhudi kufufua mbinu ilizokuwa ikitumia kuivutia Afrika wakati wa Vita Baridi vya Dunia kati ya 1947 na 1991. Mbali na uhaba mkubwa wa chakula na bei za juu za bidhaa, vikwazo vya majuzi vya kimataifa vimezua maswali kuhusu uwezo wa urusi wa kudumisha na kutimiza ahadi zake kwa baadhi ya mataifa ya Afrika.*

● Na LEVIN OPIYO

HUENDA mpango wa Urusi kuendeleza ushawishi wake barani Afrika ukagonga mwamba, kutokana na operesheni yake ya kijeshi inayoendelea nchini Ukraine.

Kando na mgogoro uliopo kuhusu uhaba wa chakula na bei za juu za bidhaa za msingi, shaka imeibuka kuhusu uwezo wa Urusi kutimiza ahadi ilizokuwa imeyapa baadhi ya mataifa ya Afrika. Kufikia sasa, Urusi inaendelea kuwekewa vikwazo vya kiuchumi na mataifa tofauti duniani, hasa barani Ulaya.

Tangu 2019, Urusi imekuwa ikifanya juhudi kufufua njia na mbinu ilizokuwa ikitumia kuivutia Afrika wakati wa Vita Baridi vya Dunia kati ya 1947 na 1991.

Wakati huo, ilibuni ujanja kuendeleza ushawishi wake barani Afrika, kwa kuharibia sifa mataifa ya Magharibi. Ilijipendekeza kama taifa linalounga mkono maslahi ya Weusi na kutumia chuki ya Afrika kwa watawala wake wa kikoloni kuvuruga mipango ya mataifa ya Magharibi barani humu.

Urusi iliunga mkono harakati za ukombozi barani humu na kutoa msaada muhimu kukwamua sekta ambazo zilikuwa zimekwama Afrika kutokana na uporaji ulioendeshwa na wakoloni. Msaada huo ulitolewa kupitia makundi ama watu binafsi. Hili halikutokana na miegemeo yao ya kisiasa, bali kwa matumaini kuwa, kupitia msaada huo, wangesaidia Urusi kuendeleza na kutimiza ushawishi wake.

Hapa Kenya, msaada huo ulitolewa kupitia mwanasiasa Jaramogi Oginga Odinga, ambaye alikuwa ameanza uhusiano na taifa hilo mnamo 1960, mara tu baada ya Kongamano la Kwanza la Jumba la Lancaster, jijini London. Kupitia kwake, Urusi ilitoa ufadhili wa masomo kwa mamia ya wanafunzi kutoka Kenya. Kando na hayo, walifa-

...Endelea Uk 26

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Afrika

# Vita vya Ukraine vyabadili biashara barani

...Kutoka Uk 25



Wapiganaji wakizima moto baada ya nyumba kulipuliwa na kombora mjini Kharkiv, Septemba 6, katika uvamizi wa Urusi dhidi ya Ukraine. PICHA | AFP

dhili shughuli tofauti za chama cha Kanu. Baada ya Kenya kupata uhuru, Jaramogi aliongoza ujumbe wa Kenya kuzuru Urusi mnamo Mei 11, 1964.

Kwenye ziara hiyo, alifanikiwa kupata msaada wa Sh370 milioni, tukio lililoshangaza sana mataifa ya Magharibi. Mataifa hayo yalifanya juu chini kukabili mwelekeo huo.

Msaada huo ulijumuisha ujenzi wa Hospitali ya Mafunzo na Rufaa ya Jaramogi Oginga Odinga na ufadhili wa miradi ya kilimo.

Hata hivyo, miradi mingi haikufaulu, kwani ilivurugwa na mataifa ya Magharibi kuhakikisha yamedumisha urafiki na uhirika wake na Kenya. Hatua ya kutengwa kwa Jaramogi kisiasa na serikali hatimaye ilivuruga na kumaliza juhudi za Urusi kuendeleza ushawishi wake nchini. Mataifa ya Magharibi pia yalichangia sana masaibu ya kisiasa yaliyomwandama Jaramogi baadaye.

Licha ya juhudi za Urusi kuvurugwa nchini, iliendelea kufurahia uhusiano mzuri na mataifa mengine barani Afrika kama Ethiopia, Angola, Msumbiji na Misri.

Vita Baridi vya Dunia vilipomalizika mnamo 1991, mahusiano hayo pia yalikatika mara moja.

Urusi ilikuwa na changamoto nyingi za kiuchumi na kisiasa ilizopaswa kushughulikia, mara tu baada ya kuvunjika kwa uliokuwa Muungano wa Mataifa ya Sovieti (USSR). Kutokana na changamoto hizo, shughuli za Urusi barani Afrika zilipungua sana. Karibu miongo mitatu baadaye, Urusi imerudi Afrika kujaribu kufufua uhusiano wa awali.

Hili ni kutokana na vikwazo vingi vya kiuchumi ambavyo imewekewa na mataifa ya Magharibi kutokana na uvamizi wake Ukraine.

Utawala wa Urusi unaona Afrika kuwa mahali ambapo taifa hilo linaweza kutumia kurudisha ushawishi wake duniani. Hali iliyoonyesha umuhimu wa Afrika kwa Urusi ni Kongamano Maalumu la Urusi na Afrika lililoandaliwa na Rais Vladimir Putin mnamo 2019 katika jiji la Sochi, nchini humo.

Kongamano hilo lilihudhuriwa na viongozi wa Afrika kutoka nchi 43. Kwa Urusi, kutafuta masoko mapya ya bidhaa zake na kupata uungwaji mkono wa kidiplomasia hasa katika Umoja wa Mataifa (UN), zilikuwa mbinu muhimu katika kufikia na kufanikisha mpango wake.

Hata hivyo, vita vipya vya Ukraine vimezua msururu mpya wa vikwazo vya kiuchumi na kisiasa, hali ambayo huenda ikaathiri uhusiano kati yake na Afrika. Kutokana na changamoto za kiuchumi na masuala mengine kuhusu mgogoro wa Ukraine, mataifa ya Afrika yamelazimika kutafuta bidhaa muhimu za matumizi kwingineko, hali ambayo imechangia bei za bidhaa muhimu kupanda sana.

Kidiplomasia, mataifa mengi yanaunga mkono Ukraine dhidi ya uvamizi wa Urusi. Hilo lilidhihirika katika UN, ambapo mataifa 28 yalipiga kura kuunga mkono Urusi kuwekewa vikwazo hivyo, huku mataifa 17 yakisusia kura hiyo.

Nigeria na Kenya ni miongoni mwa mataifa yaliyopiga kura kuunga mkono Ukraine. Kenya ilitaja uvamizi huo kuwa ukoloni ulioendeshwa barani Afrika katika karne ya 20.

Huenda hiyo ndiyo sababu Waziri wa Mashauri ya Kigeni wa Urusi, Sergei Lavrov, alikwepa mataifa hayo mawili kwenye ziara aliyofanya majuzi barani Afrika.

Kinaya ni kuwa, licha ya waziri huyo kutozuru Kenya na Uganda, nchi hizi zilitembelewa na msimamizi mkuu wa Shirika la Misaada ya Kimataifa la Amerika (USAID), Bi Samantha Power.

Ziara yake Afrika ilionekana kama juhudi za Amerika kutafuta uungwaji mkono wake dhidi ya Urusi kuhusu vita vya Ukraine. Akiwa nchini, Bi Power alimlaumu vikali Rais Putin kwa "kuleta matatizo mengi nchini na mataifa mengine kutokana na hatua ya Urusi kuzuia usafirishaji wa mbolea na nafaka kutoka Ukraine."

Hata hivyo, madai hayo yalikanushwa vikali na Lavrov, akilaumu mataifa ya Magharibi kuwa chanzo kikuu cha changamoto hizo. Aliyalaumu kwa vikwazo vya kiuchumi walivyoiwekea Urusi.

Lavrov pia aliomba UN kuyapa nguvu mataifa zaidi ya Afrika. Aliyalaumu mataifa ya Magharibi kwa kuendelea kuinyanyasa kisiasa Afrika, kwa kushinikiza nchi za bara hilo kutounga mkono Urusi.

**Kutengwa kwa Oginga ambako kulichochewa na mataifa ya Magharibi kutokana na uhusiano wake na Urusi kulitia tamati mpango wa Urusi kuendeleza ushawishi wake nchini Kenya.**

Kiwango ambacho vita vya Ukraine vimevuruga uhusiano wa Urusi na Afrika kitabainika Novemba wakati wa Kongamano la Urusi na Mataifa ya Afrika.

Kongamano hilo litafanywa wiki mbili tu kabla ya Rais Joe Biden wa Amerika kuandaa lingine kati yake na viongozi wa Afrika.

Inaelezwa kwamba, ili kuvuruga mipango ya Rais Putin barani Afrika, huenda nchi za Magharibi zikashawishi viongozi kutoka Afrika kususia kongamano la Urusi.




Mwanamke akijaribu bunduki aina ya Kalashnikov wakati wa Kongamano la Kiuchumi kati ya Urusi na mataifa ya Arika katika eneo la Black Sea, jijini Sochi, Octoba 24, 2019. PICHA | AFP

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya Dunia

■ AJALI ZA KAZINI INDIA



Wazima moto nchini India wakinyunyiza maji kuzima moto katika kiwanda cha bidhaa za kemikali karibu na eneo la Howrah Bridge, jijini Kolkata, Juni 8, 2019. PICHA IAFP

# 'VIWANDA VYA MAUTI'

*India inalenga kuwa taifa lenye ustawi wa viwanda huku sera za serikali na mageuzi mengine yakilenga kuvutia uwekezaji na ubunifu. Lakini mikasa ya moto imekuwa jambo la kawaida ambapo wafanyakazi wanyonge ndio hukiathirika zaidi.*

● DELHI

"Hiki ni kiwanda cha mauti". Mikono ya Ismail Khan inatetemeka anapoelekeza kidole katika orofa ya pili ya jengo lililochomeka katika jiji kuu la Delhi, nchini India.

Hapa ndipo alipomuona dada yake mdogo mara ya mwisho, akiwa amekwama akijaribu kujiokoa kutoka jengo hilo lililokuwa limefunikwa na moshi na moto.

Maskan, 21, alikuwa miongoni mwa watu 27 waliokufa katika moto mkubwa uliotokea Mei ndani ya chumba ambako bidhaa za kielektroniki hutengenezwa kwenye jumba hilo la orofa nne.

Siku chache baada ya kuzuka kwa moto huo, afisa wa polisi wa cheo cha juu aliambia wanahabari mwenye jumba hilo hakupata kibali cha polisi na idara ya moto kabla ya kukodisha orofa tatu za jengo hilo kwa ndugu wawili waliosimamia kiwanda hicho.

Msemaji wa polisi jijini Delhi alisema kiwanda hicho hakikuwa na leseni inayohiyajika kukiruhusu kuendesha shughuli.

Tulimpigia simu mmiliki wa kiwanda hicho mara kadhaa lakini hakujibu. Tulijaribu pia kumfikia wakili wake lakini alikataa kutupa maelezo kuhusu mahala kwa kuelekeza maswali yetu.

India inalenga kuwa taifa lenye ustawi wa viwanda huku sera za serikali na mageuzi mengine yakilenga kuvutia uwekezaji na ubunifu.

Lakini mikasa kama huo wa moto jijini Delhi hutokea kila wakati, na wafanyakazi ndio huathirika zaidi.

Ajali za viwandani huua mamia ya watu na kulemaza maelfu ya wengine kila mwaka.

Waziri wa jimbo moja aliambia Bunge mnamo 2021 kuwa wafanyakazi wapatao 6,500 walikufa wakifanya kazi katika viwanda, bandari, migo-

...Endelea Uk 28

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Dunia

# Ndani ya viwanda vya mauti nchini India



Wazima moto nchini India wakizima moto uliozuka katika kiwanda cha mafuta eneo la Ajmer, jijini Rajasthan, India mnamo Juni 2. PICHA | AFP

## 3,955

Hakuna data rasmi kuhusu wafanyakazi waliopata ulemavu kutokana na ajali za viwandani. Lakini uchunguzi wa majuzi wa shirika la kibinafsi unaonyesha ajali 3,955 zilitokea kati ya 2016 na 2022.

...Kutoka Uk 27

di na maeneo ya ujenzi katika miaka mitano.

Wanaharakati wa kutetea haki za wafanyakazi walisema huenda idadi ya waliokufa ni zaidi kwa sababu ajali nyingi hazijaripotiwa au kurekodiwa.

Kulingana na data iliyokusanywa na chama cha wafanyakazi ulimwenguni, vifo vingi India hutokea katika viwanda vya kuunda bidhaa za nyumbani, kemikali na maeneo ya ujenzi.

Mnamo 2021 pekee, inasemekana ajali saba ziliripotiwa kila mwezi katika viwanda vya kutengeneza bidhaa, ambapo wafanyakazi 162 walikufa.

Ndani ya miaka kadhaa, ripoti mpya zimeeleza kuwa wafanyakazi katika viwanda vidogo visivyosajiliwa ndio huathiriwa zaidi na ajali za viwandani.

Waathiriwa huwa wafanyakazi masikini au wahamiaji ambao familia zao hazina rasilimali za kugharamia kesi mahakamani kupigania fidia.

Rakesh Kumar anaamka usiku wa manane akipiga mayowe. Alipoteza binti zake wawili katika mkasa wa moto uliotokea katika kiwanda kimoja jiji Delhi wanakotengeneza nyaya za Wi-Fi. Wanalipwa mshahara wa dola 100 (karibu Sh12,000) kwa mwezi. "Binti zangu waliathirika zaidi," akasema.

Familia ilisubiri habari kuwahusu siku kadhaa baada ya mkasa huo wa moto. Hatimaye polisi waliwaita wafanyiwe vipimo vya DNA kutambua mabaki ya wapendwa wao yaliyochomeka kiasi cha kutoweza kutambuliwa.

Mnamo Agosti, polisi wa Delhi walipeleka mashtaka kortini dhidi ya watu watano walioshukiwa kuanzisha moto.

Mashtaka hayo yanajumuisha jaribio la kuua watu au kusababisha kifo kwa kutokuwa mwangalifu.

Rajeshi Kashyap, mwanaharakati wa chama cha kutetea wafanyakazi jijini Delhi, anadai viwanda vingi katika jiji kuu na viungani huvunja kanuni kadhaa za usalama. Lakini maafisa wa serikali hawachukuia hatua zozote za kinidhamu dhidi ya wamiliki wa viwanda hivyo.

Yeye na wanaharakati wenzake wanadai wamiliki viwanda wachache wanaokamatwa kwa kukiuka sheria na kanuni, huachiliwa kwa dhamana au kesi dhidi yao kujivuta kotini kwa muda mrefu.

Kulingana na polisi, ajali 663 za viwandani zilirekodiwa jijini Delhi ndani ya miaka mitano iliyopita, ambapo watu 245 walikufa. Karibu watu 84 walikamatwa kuhusiana na ajali hizi.

Wakijitetea dhidi ya tetesi za wanaharakati hao kwamba uchunguzi kuhusu visa hivyo huendesha visivyo, polisi wanasema wanajaribu kuhakikisha "hatua zimechukuliwa dhidi ya wahusika."

Tulikutana na familia nyingi zimejawa na huzuni baada ya kupoteza wapendwa wake, wengi wakiwa tegemeo lao.

Lakini masharti ya kisheria na sababu nyingine zimezima juhudi za familia za marehemu kupata fidia kutoka kwa viwanda hivyo.

Wakili mashuhuri, ambaye ameshughulikia kesi nyingi za kudai fidia kwa wafanyakazi waliokufa katika ajali za viwandani, anasema kesi aina hiyo hujivuta kwa miaka mingi.

"Wafanyakazi hawana imani na mfumo wa sheria. Wengi huchukua pesa kidogo wanazolipwa fidia na serikali na kuondoka," anasema Chandan Kumar, mmoja wa viongozi wa mashirika ya umma yanayosaidia wafanyakazi wa viwanda vidogo.

Tulijaribu kufikia familia za waathiriwa wa mkasa wa moto katika kiwanda kimoja jijini Delhi 2018 ambapo wafanyakazi 17 walikufa. Lakini karibu wote walikuwa wameondoka jijini humo na kuhamia vijijini au katika miji mingine kutafuta kazi zingine.

Sangeeta Roy, 50, alipoteza mkono akitumia mashine ya kukata mbao kiwandani miaka mitatu iliyopita.

Anasema hakupokea fidia yoyote kutoka kwa waajiri wake na alilazimika kusubiri miaka mitatu kabla ya kupata malipo yanayotolewa na serikali kwa wafanyakazi wanaoumia wakiwa kazini.

Hakuna data rasmi kuhusu wafanyakazi waliopata ulemavu kutokana na ajali za viwandan. Lakini uchunguzi wa majuzi wa shirika lisilochuma la faida la "Safe in India Foundation." Unaonyesha kuwa, katika viwanda vya kutengeneza vipuri vya magari kaskazini mwa India, ajali 3,955 zilitokea kati ya 2016 na 2022.

Asilimia 70 ya waliojeruhiwa walipoteza vidole au kuumizwa mikono na mashine za kukata vyuma.

India ni kitovu cha utengenezaji magari na vipuri katika eneo pana la Asia Kusini, ikiajiri zaidi ya wafanyakazi milioni 10.

Shughuli kubwa za utengenezaji huendeshwa na kampuni ndogo ndogo.

India imeanza kutekeleza mageuzi katika sheria zake za leba hasa zinazohusiana na usalama na afya ya wafanyakazi na usalama wa mazingira ya kufanyia kazi.

Lakini wanaharakati wa kutetea maslahi ya wafanyakazi wameelezea hofu kuwa huenda viwanda vingi vikakataa kutekeleza sheria hizo mpya.

Huku sheria ya zamani ikisema kampuni yoyote yenye wafanyakazi 10 na zaidi sharti iwe na kamati ya usalama, sheria mpya iliyopendekezwa imeongeza idadi ya wanachama wa kamati hiyo hadi 250.

Wafanyakazi wengi pia wanachelea kujiunga na vyama vya kutetea maslahi yao kwa hofu ya kupoteza nafasi za ajira.

Serikali pia imebadilisha kanuni au utaratibu wa ukaguzi wa maeneo ya kazi ili kampuni ziweze kuendesha shughuli hiyo kwa urahisi.

Ingawa wakati huu maafisa wa leba ndio hukagua sehemu za kazi kuhakikisha kuwa zinaafisa kanuni za usalama zilizowekwa, wajibu wao utabadilika na kuwa wa wapatanishi chini ya kanuni mpya.

Wataalamu wa masuala ya leba wanasema mabadiliko hayo yatafanya wenye viwanda kutoupa kipaumbele usalama wa wafanyakazi.

"Hatimaye usalama wa wafanyakazi hautakuwa jukumu la yeyote," anasema Sidheshwar Prasad Shukla, msomi na mwanaharakati wa kutetea masilahi ya wafanyakazi.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Dunia

■ KUTENGWA NA KUFUNGIWA KWA WATU



Picha iliyopigwa angani ikionyesha mahabara zilizojengwa kwa hewa iliyopulizwa jijini Chengdu in, China. Jiji la Chengdu limejenga mahabara tano za aina hiyo vya kupima virusi vya Covid-19, na kupanua uwezo wake wa kupima virusi hivyo hadi vipimo 250,000 kwa siku. PICHA NDOGO: Mhudumu wa afya akichukua kipimo kutoka kwa mwanamume ili kukikagua. PICHA | AFP

# COVID YAPONDA CHINA

*Miji zaidi ya 70 nchini China ilifungwa kabisa ama sehemu zake tangu wa Agosti, " na kuathiri watu zaidi ya 300 milioni huku maafisa wa serikali wakijitahidi kukabili maambukizi mapya kwa kila hali, kiongozi wa nchi hiyo Xi Jinping akitarajiwa kuanza muhula wa tatu.*

• Na KWENDO OPANGA

Mataifa yenye nguvu zaidi kiuchumi duniani, Amerika na China, hayaonani ana kwa ana, hata kunapozuka janga ulimwenguni linalohitaji kukabiliwa kwa pamoja. Amerika, ambayo ina watu 300 milioni, iliathiriwa zaidi na janga la virusi vya corona kuliko China, iliyo na watu 1.4 bilioni.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), kufikia Septemba 5, China ilikuwa imeripoti visa 6,588,896 vya maambukizi ya virusi vya corona, na vifo 25,019 tangu Januari 2020.

Shirika hilo pia liliripoti kuwa, wakati huo huo, Amerika ilikuwa imeripoti maambukizi 93,332,054 na vifo 1,035,674. Lakini mikakati ya mataifa haya mawili ya kukabiliana na virusi vya corona ilikuwa tofauti sana.

Katika wiki moja iliyopita, serikali ya China ilifunga wa Chengdu, kusini magharibi mwa China, wanamoishi watu 21 milioni.

Maambukizi mapya 157 e zilizotangulia na Chengdu ukawa mji wa hivi punde wa China kufungwa kuambatana na sera ya nchi hiyo ya kuangamiza covid kabisa.

Mnamo Jumatatu, shirika la habari la CNN liliripoti kuwa miji zaidi ya 70 nchini China ilifungwa kabisa ama sehemu zake tangu wa Agosti, " na kuathiri watu zaidi ya 300 milioni huku maafisa wa serikali wakijitahidi kukabili maambukizi mapya kwa kila hali, kiongozi wa nchi hiyo Xi Jinping akitarajiwa kuanza muhula wa tatu.

Shirika hilo, likinukuu jarida la kifedha la China, Caixin, pia liliripoti kuwa miji isiyopungua 33 kwa sasa imefungwa kabisa ama sehemu zake na mingine mingi huenda ikafuata hivi karibuni.

Hiyo ina maana kuwa huenda China haiko tayari kuishi na Covid-19, kama Ulaya, Amerika na sehemu nyingi za ulimwengu.

China ndiyo nchi pekee ulimwenguni inayozingatia sera ya kufunga miji na maeneo mengine katika vita vyake dhidi ya Covid-19. Mayaifa yameamua kuishi na ugonjwa huo na kulegeza au kuondoa kabisa masharti makali ambayo yaliwekwa corona ilipozuka China miaka mitatu iliyopita.

Sera ya China ya kuangamiza kabisa Covid inahusisha kutengwa na kufungiwa kwa watu katika maeneo yaliyo na visa vingi vya maambukizi, watu wengi kupimes na wanaotangamana na waathiriwa kutambuliwa, kuruhusu mtu mmoja tu kutoka kila familia kutoka nje kununua bidhaa muhimu na kufungwa kwa maeneo ya burundani.

Nchi nyingi zilichukua mwelekeo wa kutumia chanjo kupambana na corona ilipotangazwa janga mwaka wa 2020 kisha zikalegeza masharti baada ya kugundua kwamba Covid-19 itadumu kwa miaka mingi kwa hivyo ni janga la kuishi nalo.

Lakini China inaonekana kuwa tayari kuendeleza mpango wa kufunga maeneo kuangamiza covid hadi wakati usiojulikana.

**Mataifa yote duniani yameingia katika awamu ya kuishi na ugonjwa huo na kuelegeza ama kuondoa kabisa masharti makali yaliyowekwa punde tu baada ya corona kutokea nchini China miaka mitayu iliyopita.**

Hata hivyo, upinzani kwa sera hii unaongezeka. Mnamo Agosti 28, Taasisi ya Utafiti ya Anbound nchini China, ilitangaza tofauti isiyo ya kawaida kati ya China na chama cha Kikomunisti ikisema sera ya kufunga miji ili kumaliza covid, ni lazima iondolewe ili kuzuia kulemaa kwa uchumi.

Katika taarifa yake yenye kichwa "Ni Wakati wa China Kubadilisha Sera zake za Kuzuia na Kuthibiti Virusi, taasisi hiyo ilishauri kuwa kuzuia uchumi kulemaa kunafaa kupewa umuhimu China, sawa na ilivyo Amerika, Japan na Ulaya.

Televisheni ya WION iliripoti kuwa taarifa ya Anbound iliwekwa katika akaunti zake za mtandao maarufu wa kijamii wa WeChat na katika blogu ya Sina Weibo, lakini ikaondolewa Jumatatu adhuhuri.

Ni wazi kuwa hata kama China inafikiria kubadilisha mbinu yake wa kupigana na covid, haikuchukulia vyema ushauri kutoka Anbound.

Ni muhimu kutambua kuwa Anbound ilikita ushauri wake dhidi ya kufunga miji katika kupungua kwa ukuaji wa uchumi China, na biashara muhimu kati ya nchi hiyo na mataifa mengine ulimwenguni.

Huku wataalamu wakilaumu kufifia kwa uchumi wa China kutokana na kufungwa kwa miji na maeneo mengine, serikali ya nchi hiyo inalaumu virusi hivyo wala si mkakati wake wa kupigana navyo kwa kufifia kwa uchumi.

Waangalizi wa nchi za Magharibi, wanataja milipuko ya corona katika maeneo ya China yakiwemo yaliyowahi, kuwa ushahidi kwamba mkakati wa China wa kumaliza covid kabisa umeshindwa au kufunga maeneo si suluhisho.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

TANZIA

■ MAISHA MAREFU YENYE UWAJIBIKAJI



# MALKIA WA MIAKA NA MIKAKA

Utawala wa kipindi kirefu cha Malkia Elizabeth II uliongozwa na nia ya kutekeleza majukumu yake na kujitolea kwa matakwa ya wadhifa wake na raia wa Uingereza.

Japo ushawishi wa Uingereza ulibadilika, kulingana na mabadiliko ulimwenguni, ushawishi wa Malkia Elizabeth II ulisalia. Alifaulu kudumisha mshikamano katika ufalme wa Uingereza hata nyakati ambapo nchi hiyo ilikumbwa na changamoto nyingi.

Alipozaliwa hakuna aliyedhani kuwa angepanda ngazi hadi kuwa kiongozi wa taifa hilo linalokumbatia uongozi wa kifalme.

Malkia huyo ambaye jina lake halisi ni; Elizabeth Alecandra Mary Windsor alizaliwa mnamo 1926 katika nyumba moja kando ya eneo la Berkeley Square jijini London.

Alikuwa kifua mimba wa Albert ambaye, alitambuliwa kama "Duke of York" ( yaani kiongozi wa mji wa York). Albert alikuwa mwana kiume wa Mfalme George V na mkewe, Elizabeth Bowes-Lyon.

Elizabeth na dadake, Margaret Rose, ambaye alizalishwa 1930, walisomeshwa nyumbani na kulelewa katika familia yenye upendo.

Elizabeth alikuwa na uhusiano wa karibu zaidi na babake, Albert, na babu yake, Mfalme George V.

Alipotimu umri wa miaka sita, Elizabeth alimwambia mkufunzi wake, wa uendeshaji baiskeli, kwamba alitaka kuwa "kiongozi wa nchi mwenye farasi na mbwa wengi."

Inasemekana kuwa alionyesha sifa za uongozi na uwajibikaji akiwa na umri mdogo. Winston Churchill, ambaye baadaye alihudumu kama Waziri Mkuu wa Uingereza, alinukuliwa akisema kuwa Elizabeth alionyesha sifa za "kimamlaka za kushangaza kuwahi kushuhudiwa katika mtoto mdogo."

Japo hakuwahi kuhudhuria shule, Elizabeth alithibitisha uwepo wa kipekee wa umilisi wa lugha mbalimbali na baadaye alisomea historia ya utayarishaji Katiba.

Kikosi maalum cha maskauti wa kike, Girl Guides, katika Kasri ya Buckingham, kilibuniwa kusudi Elizabeth aweza kutangamana na wasichana wa umri wake.

Kifo cha Mfalme George V mnamo 1936, kifungua mimba chake, kwa jina David, alichukua usukuni kuwa Mfalme Edward VIII.

Hata hivyo, mke wake, Wallis Simpson, mwanamke raia wa Amerika ambaye aliwahi kutalikiwa mara mbili, alikataliwa kutokana na sababu za kisiasa na kidini.

Mwishoni mwa mwaka huo alighairi majukumu ya kifalme. Badaye "Duke of York" (msimamizi wa mji wa York) alipandishwa cheo na kuwa Mfalme George VI.

Kutawazwa kwake kulimpa Elizabeth uelewa wa mapema kuhusu majukumu ambayo yalikuwa yakimsubiri. Baadaye aliandika kwamba alibaini kuwa huduma za kifalme "zilikuwa nzuri zaidi."

Kwa msingi ya taharuki zilizogubika bara Ulaya nyakati hizo, Mfalme mpya, pamoja na mkewe Malkia Elizabeth, walijitolea kurejesha imani ya umma kwa ufalme huo.

Mfano wao uliigwa na binti wao mkubwa. Mnamo 1939, binti mfalme aliyekuwa na umri wa miaka aliandamana na Mfalme na Malkia kuzuri Taasisi ya Mafunzo ya Wanajeshi wa Kikosi cha Wanamaji, Royal Naval College, katika Dartmouth.

Pamoja na dadake Margaret, alisindikizwa na mmoja wa maafisa wa cheo cha Cadet, binamu wake, Mwana Mfalme Philip wa Ugriki.

Haikuwa mara ya kwanza kwa wao kukutana, lakini ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Elizabeth kuvutiwa na Philip.

Philip aliwaita jamaa zake alipokuwa likizoni na mnamo 1944 alipokuwa na umri wa miaka 18, Elizabeth alionyesha wazi kumpenda (Philip). Alihifadhi picha ya Philip katika chumba chake na waliandikiana barua.

Elizabeth alijiunga na kikosi cha ziada cha Auxiliary Territorial Service (ATS), wakati ambapo Vita vya Pili vya Dunia ambako alijifunza kazi ya kuendesha na kukarabati magari.

Baadaye, alijiunga na Familia ya Kifalme katika Kasri la Buckingham huku maelefu ya watu wakijikusanya kuadhimisha mwisho wa vita barani Uropa. "Tuliuliza wazazi wangu ikiwa tungetoka nje ili tushuhudie sherehe hizo," alikumbuka.

"Nakumbuka kuwa tuliogopa kutambuliwa. Nakumbuka foleni ndefu ya watu wasiojulikana wakishikana mikono wakitembea kutoka ukumbi wa Whitehall. Sote tulifurahi." akaongeza.

Baada ya vita, hamu ya Elizabeth kuoana na Mwana Mfalme Philip ilikumbwa na changamoto. Mfalme hakuwa tayari kumpoteza bintiye aliyemuenzi. Na ilimlazimu Philip kukabiliana na dhana katika familia hiyo ambayo haikuwa tayari kumkubali kwa misingi kuwa alitoka kizazi kigeni.

Lakini hatimaye matamanio ya Elizabeth na Philip yalizingatiwa na mnamo Novemba 20, 2047 wawili hao walifunga ndoa katika eneo la Westminster Abbey.

Msimamizi wa mji wa Edinburgh, jinsi ambavyo Philip alijulikana, alisalia kuwa mwanajeshi wa kikosi cha wanamaji.

Kuhamishwa kwake hadi mji wa Malta kuliwapa nafasi ya kufurahia maisha ya kawaida. Mtoto wao wa kwanza, Charles, alizaliwa mnamo 1948, akafuatwa na dadake, Anne, aliyezaliwa mnamo 1950

Lakini kwa sababu Mfalme alikabiliwa na changamoto nyingi katika miaka ya vita, alipatwa na ugonjwa wa kansa ya mapafu.

Hii ni kutokana na uraibu wake wa uvutaji sigara miaka mingi maishani mwake. Mnamo 1952, Elizabeth, wakati huo akiwa na umri wa miaka 25, aliondoka na Philip kwa ziara ya ng'ambo.

Mfalme, naye, kinyume na ushauri wa madaktari, aliwasindikiza hadi uwanja wa ndege. Ilikuwa ni siku ya mwisho kwa Elizabeth kumwona babake akiwa hai.

***–BBC***


ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# *The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore*

## anywhere, anytime.

Follow the link to subscribe

> ***epaper.nation.africa.***




Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play

Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111

Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION → ePaper

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep




**SMS the word GAZETI to 20567,**
Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE SMS text and FREE Delivery**

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

Terms & Conditions apply*